SUPA JACKPOT
TZS. 1,139,859,317
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**BAKWATA** yatua mikoani kukemea ushoga, kuyumba maadili ya jamii

UKURASA 3



**ROBERTINHO AKIRI ANA WAKATI MGUMU**

UKURASA 23


# Nipashe

Alhamisi Agosti 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581391

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Gari, vifaa CHADEMA vyapigwa kibiriti Chato

## LISSU atoa kauli nzito, aendelea na mikutano...

*Endelea Uk. 2*










Tundu Lissu

Picha tofauti zikionesha sehemu za gari la matangazo la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), lenye namba za usajili T658 DQL, baada ya kuchomwa moto na watu wasiojulikana katika hoteli ya Twiga, mjini Chato usiku wa kuamkia juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makali ya maisha kupaa bei mafuta

**WASAFIRISHAJI** waitana wapandishe nauli *Endelea Uk. 2*




UKURASA WA 4

**WANASHERIA: RUKHSA MJADALA MKATABA WA DP WORLD**

BAADA ya mjadala wa makubaliano ya uwekezaji bandarini baina ya Serikali ya Tanzania na Dubai...

UKURASA WA 8

**DADA WA KAZI KIZIMBANI MASHTAKA KUINGILIA MFUMO NA KUIBA MIL. 13.8/-**

MFANYAKAZI wa ndani, Riziki Kanena (22), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar...


# Miili ya watoto 14 waliokufa maji ziwani yaopolewa

UKURASA 3


**MICHEZO** MSHAMBULIAJI YANGA AOMBA MUDA KUONYESHA MAKALI YAKE UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Akinamama wa kitongoji cha Mnazi, kijiji cha Kwamwande, kata ya Bokwa, wilayani Kilindi mkoani Tanga, wakishirikiana kusonga ugali kwa ajili ya wananchi waliyohudhuria moja ya sherehe kitongojini hapo hivi karibuni. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Gari, vifaa CHADEMA vyapigwa kibiriti Chato

**Na Vitus Audax**

GARI la matangazo na vifaa vya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) vimechomwa moto usiku mjini Chato, mkoani Geita.

Licha ya tukio hilo, pia madai ya kuwapo vitisho kiusalama, uongozi wa juu wa chama hicho umesema utaendelea na mikutano yake ya kisiasa mkoani Geita, ili kufikisha ujumbe iliokusudia kwa wananchi.

Mbali na kudai kuchomewa gari lao la matangazo na vifaa, uongozi wa chama hicho pia umedai uhalifu huo uliofanyika usiku wa kuamkia jana, pia kuna madai ya baadhi ya watu wanaokipa ushirikiano, wanatishiwa kuharibiwa mali zao.

Jana, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu, alipozungumza na Nipashe kwa simu, alitaja vikwazo dhidi yao mkoani Geita vinajumuisha kuchomwa moto kwa gari lao la matangazo.

"Kabla ya tukio la jana (juzi usiku), kuna sehemu tulikwenda kukodi vifaa vya muziki, tukakubaliana gharama, lakini cha ajabu akapigiwa simu na kuelezwa kuwa endapo akitoa vifaa hivyo, vitateketezwa kwa moto. Kijana huyo akatupigia na kusema hatoweza kufanya hivyo," Lissu alidai pasi na kutaja jina wala taasisi iliyomtishia kijana huyo.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema kutokana na kukumbana na kikwazo hicho, walishindwa kupata vifaa hivyo, hivyo kulazimika kutumia vifaa vya chama kufanya matangazo katika maeneo mbalimbali na baada ya matangazo, waliomba maegesho katika moja ya hoteli za mjini Chato, akiitaja jina.

Alidai kuwa katika maegesho ya hoteli hiyo, kulikuwa na magari mengine matano ya watu binafsi. Gari lenye namba za usajili T 658 DQL, mali ya CHADEMA, lilichomwa moto saa 1:10 usiku wa kuamkia jana.

Alilitaja kuwa walilitumia katika mkutano wao wa hadhara uliofanyika juzi katika Jimbo la Mbogwe, mkoani Geita.

"Pia, vifaa vya matangazo vimechomwa moto. Si hilo tu, wakati huu (jana mchana) nimepokea taarifa ya kuchomwa moto kwa jukwaa lililoandaliwa kwa ajili ya mkutano wetu katika Kata ya Muganza, wilayani Chato," alisema.

Alihusisha matukio hayo na kauli za baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) alizoziita za uchochezi dhidi ya CHADEMA, akirejea kauli ya mmoja ya wajumbe wa Kamati Kuu ya CCM aliyoitoa Julai 30 katika mkutano wa chama hicho mkoani Mwanza.

Lissu alisema licha ya vikwazo hivyo hawatokata tamaa. Wataendelea na mikutano yao ndani ya Chato kama ilivyopangwa. Hakuna kurudi nyuma!

"Haijalishi vyombo vya matangazo na majukwaa yanachomwa moto, tutafanya mikutano yetu kwa gharama yoyote hata kwa kupanda juu ya 'pickup'. Niwatake wanachama na wananchi kwa ujumla - wasikate tamaa wala wasitishwe na vitendo hivyo vya kihuni na siasa chafu zinazoendelea kufanyika," alisisitiza.

Kuhusu ushirikiano wa Jeshi la Polisi katika kushughulikia matukio hayo, Lissu alisema walifanya mawasiliano na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita pamoja na wasaidizi wake na kuwahakikishia kuwaongeza ulinzi katika mikutano yao yote ya hadhara wanayoendelea kuifanya mkoani mwake.

**HOJA YA MATUSI**

Alipoulizwa kuhusu tuhuma zinazoelekezwa kwao kutumia lugha ya matusi dhidi ya viongozi wa CCM na serikali, Lissu aliitaja ni propaganda dhidi yao.

Alisema hakuna sehemu ambako wanaongea matusi na wamekuwa wakiambiwa hivyo miaka mingi, ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani ambako wanaoeneza propaganda hiyo walishindwa kuthibitisha matusi hayo.

Jana jioni, Lissu alihutubia mkutano wa hadhara mjini Chato, akieleza sababu za chama hicho kupinga mkataba wa bandari na kampuni ya DP World ya Dubai. Alionya kuwa kinachoshuhudiwa sasa kwenye sekta ya madini - migodi inamilikiwa na wageni, ndicho wanachokikataa kufanyika katika bandari.

Katika taarifa yake kwa umma jana, Katibu wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), Yohana Kaunya ambaye juzi alikuwa sehemu ya waliotumia gari hilo la matangazo 'lililopigwa kibiriti', alisema kuwa baada ya kuchomwa moto, waliolichoma walianza kuwatafuta dereva na mpiga muziki (DJ) wa chama hicho, wakidai "zamu yao inafuata", lakini hawakufanikiwa kuwapata.

Alisema kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliwahi eneo la tukio na kuzima moto huo kabla gari hilo halijateketea lote, akikiri kumepawa ushirikiano toka Jeshi la Polisi mkoani Geita.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Wilaya ya Chato, Pamphili Hwago, alinukuliwa katika mazungumzo na vyombo vya habari akisema Lissu asipoomba radhi juu ya kauli zake kwa viongozi wa CCM na serikali, hatoruhusiwa kukanyaga ardhi ya Chato.

Vilevile, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Stephen Wasira, akiwa katika mkutano wa chama mkoani Mwanza mwishoni mwa mwezi uliopita, aliwataka wana CCM wilayani Chato kumzomea Lissu atakapofanya mikutano yake wilayani humo. Alidai Lissu ni mwongo.

## Makali ya maisha kupaa bei mafuta

**Na Jenifer Gilla**

BEI ya mafuta mwezi huu imepandishwa. Tangazo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) la jana limeelekeza bei mpya za mafuta zinazoonesha bei za petroli na dizeli zimepanda.

Sababu kuu ya ongezeko hilo ni changamoto katika upatikanaji wa dola nchini na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya sarafyu hiyo ya kigeni.

EWURA pia imetaja mabadiliko ya sera kikodi, ongezeko la gharama ya mafuta katika soko la dunia na gharama za uagizaji wa mafuta kuwa ni sababu nyingine ya kupanda kwa bei ya nishati hiyo nchini.

Bei mpya ya jumla ya mafuta ya petroli itakayotumika kuanzia jana imeongezeka kwa Sh. 461.36 huku dizeli ikipanda kwa Sh. 391 kwa Dar es Salaam.

Kwa Mkoa wa Tanga, bei ya petroli imepanda kufikia Sh. 2,985 na kutoka Sh. 2,593.92 ya mwezi Julai sawa na ongezeko la Sh. 392, huku dizeli ikiuzwa Sh. 2,849.8 kutoka 2,628 sawa na ongezeko la Sh. 221.

Mkoani Mtwara bei za mafuta hazijaongezeka. Ikiendelea kuwa Sh.2,662.38 kwa petroli na Sh. 2,867.94 kwa dizeli.

Bei mpya za mafuta hayo kwa rejareja mkoani Tanga, petroli itakuwa Sh. 3,245 kutoka Sh. 2,724, mwezi uliopita huku dizeli ikiuzwa Sh. 2,981 kutoka Sh. 2,760 mwezi uliopita, Mtwara petroli itauzwa Sh. 3,271 kutoka Sh. 2,809 na dizeli ni Sh. 3,008 kutoka Sh. 3,000.

Mikoa itakayonunua mafuta hayo kwa bei ya juu ya rejareja nchini ni Kagera ambayo sasa wateja walioko wilayani Bukoba watanunua petroli kwa Sh. 3,415 kutoka Sh. 2,952 mwezi uliopita, wakati wilayaya Kyerwa wateja wake watanunua dizeli kwa Sh. 3,173 ikiwa ya juu zaidi nchini.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Joseph Priscus, alisema ongezeko hilo litaathiri kwa kiasi kikubwa biashara zao kwa kuwa mafuta yanachukua asilimia 75 ya gharama za uendeshaji.

"Kutokana na uharaka na umuhimu wa jambo hili, hivi karibuni tutaanza michakato wa kupandisha nauli kwa sababu bila ya kufanya hivyo baadhi ya kampuni zitashindwa kuendelea na biashara," alisema Joseph.

Alitoa mfano kuwa kwa bei hizo mpya, kampuni yenye mabasi 10 yanayokwenda safari ndefu itapata hasara ya Sh. milioni 60 kwa wiki, huku kampuni yenye mabasi 10 yanayotumia njia ya Dar es Salaam-Dodoma itapata hasara ya Sh. milioni nne kwa siku.

Alitoa wito kwa serikali kurejesha ruzuku ya serikali katika mafuta ili kuwaepusha wafanyabiashara dhidi ya alichokiita machungu ya kupanda kwa bei ya mafuta.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Mkoa wa Dar es Salaam (DACOBOA), Sabri Mabrouk, alisema inasikitisha kuona biashara ya usafirishaji imeathiriwa na uhaba wa dola. Gharama za uendeshaji wa biashara hiyo zimepanda.

Meneja usafirishaji kutoka kampuni ya Yaate Investment Limited, Sadock Tuya, alisema uhaba wa dola umesababisha kupungua bidhaa za kusafirisha, hali inayoathiri biashara zao.

"Kwa mfano, tulikuwa tunapata dola 5,000 kwa ajili ya kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam hadi Kasumbalesa, mpakani mwa Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), lakini sasa tunapata dola 4,400 kwa mafuta yale yale yaliyotumika jambo ambalo halina faida," alisema.

HABARI KITAIFA

# Miili ya watoto 14 waliokufa maji Ziwa Victoria yaopolewa

**Na Jackline Masinde,** BUNDA

MIILI ya watu 13 imeopolewa usiku wa kuamkia jana kati ya 14 waliozama Ziwa Victoria karibu na Kijiji cha Mchigondo Wilaya ya Bunda mkoani Mara kutokana na ajali ya mitumbwi miwili.

Idadi hiyo ya miili iliyoopolewa jana inahitimisha kazi ya uopoaji wa miili yote 14 baada ya mwili mmoja kuopolewa Jumapili iliyopita siku ajali ilipotokea.

Miili yote ni ya watoto na kazi ya uopoaji iliendelea usiku wa kuamkia jana mpaka majira ya asubuhi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na wavuvi wilayani humo.

Ajali hiyo ilihusisha waumini wa kanisa la Mungu wa Kiroho (KTMK) ambayo idadi ya watu waliohusika kwenye ajali hiyo ni 28 huku chanzo kikitajwa kuwa ni kubadilika hali ya hewa ziwani iliyosababisha upepo na mawimbi makali.

Akithibitisha kuopolewa kwa miili hiyo, Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mara, Agustine Magere, alisema idadi kubwa ya watu waliopolewa walikuwa ni watoto wa umri kati ya mwaka mmoja, 9 na 12.

Alisema baadhi ya watoto hao ni wanafunzi kutoka Shule ya Msingi Bulomba na kati yao 14 waliokolewa na kukimbizwa hospitali na hali zao zinaendelea vizuri.

Alisema shughuli ya uopoaji miili ilikuwa ngumu kutokana na eneo hilo kuwa na tope jingi na giza lakini lilifanikiwa kwa asilimia mia moja.

Akizungumza wakati wa upoaji wa miili hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vicent Naano, alisema kupitia tukio hilo wamejifunza kuwa Jeshi la Zimamoto bado lina kazi kubwa ya kufanya ili kuongeza ufanisi katika shughuli za majanga.

Dk. Naano alisema katika tukio hilo kumeonekana uzembe wa wazazi kutofatilia usalama wa watoto na kuwaacha kwenda mahala popote bila kuwahakikishia usalama na mmiliki wa kanisa la (KMTK) ambaye aliruhusu watoto kupanda kwenye mitumbwi bila kujali usalama wao. "Kutokana na uzembe huu ninaviagiza vyombo vya dola kuwasaka wamiliki wa vyombo hivi na mchungaji wa kanisa wakamatwe kwa kosa la uzembe na kutozingatia sheria na taratibu za kupandisha watu kwenye mitumbwi ambayo hairuhusiwi kwa kazi ya usafirishaji wa abiria," alisema Dk. Naano.

Akitoa salamu za pole kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Saidi Mtanda alisema, wameandaa utaratibu wa kusafirisha miili yote kwenda kuzikwa.

Kadhalika, alisema kila familia iliyopoteza ndugu itapatiwa Shilingi milioni moja kama sehemu ya rambirambi na kuwataka wananchi kuendelea kuwa wavumilivu katika kipindi hicho kigumu.

"Serikali itaendelea kuwa karibu na familia ya ndugu zetu hawa na tutatoa vyombo vya usafiri kuhakikisha miili inafika pale wanapostahili kwenda, lakini tunaendelea kutoa pole kwa wote waliofikwa na msiba huu," alisema Mtanda.

Miili hiyo imepatikana siku ya nne tangu kuzama kwa mitumbwi hiyo na baadhi ya ndugu wa marehemu na mashuhuda walionusurika katika ajali hiyo walieleza masikitiko yao juu ya tukio hilo, akiwamo Baraka Jumbura, aliyenusurika kuwa safari yao ya kwenda haikuwa na misukosuko yoyote lakini wakati wa kurejea walikutana na dhoruba ya mawimbi mawili yalíyopiga na kujaza maji kwenye mtumbwi.

"Waliokuwa kwenye mtumbwi wa nyuma walituomba msaada baada ya mtumbwi wao kupinduka na tulivyorudi wote walilazimisha kupanda mtumbwi wa pili hali iliyosababisha nao kupinduka," alisema Jumbura

# BAKWATA yatua mikoani kukemea ushoga na kuyumba maadili ya jamii

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

ONGEZEKO la mmomonyoko wa maadili kwa jamii nchini, ikiwemo matendo ya ubakaji na kushamiri kwa vitendo vya ushoga, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), limeanza kuzunguka nchi nzima kutoa elimu na kukemea matendo hayo kwa waumini wake na kuwataka kuishi kwa kadri ya mafundisho ya dini.

Mkurugenzi wa Da'awa na Tabligh kutoka Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Arif Surya, alisema hayo jana wakati akizungumza na waumini wa Kiislam baada ya kukamilisha Ibada ya Ijitimai iliyoambatana na Dua maalum ya kuliombea taifa katika msikiti Mkuu wa Wilaya ya Tunduru.

Kwa mujibu wa Shekh Surya, Ibada hiyo imefanyika kwa siku tatu kwa viongozi wa BAKWATA kuzunguka kwenye vijiji mbalimbali kutoa mafundisho kwa waumini wao.

Alisema ibada hiyo ni mwendelezo wa viongozi wa Dini ya Kiislam wakiongozwa na Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Dk. Abubakar Zubery, kuweka kukemea matendo maovu yanayoanza kushamiri kwa kasi kubwa nchini ambayo ni kinyume cha mafundisho ya dini hiyo na maagizo ya Mwenyezi Mungu.

Alisema baadhi ya watu kutoka mataifa ya nje wanafanya jitihada kubwa kinyume cha maadili na mafundisho ya MwenyeziMungu kwa kuwafundisha watoto wa kiume kujiingiza kwenye ndoa za jinsia moja.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, alitoa wito kwa kwa viongozi wa dini, kimila na wazazi wilayani hapa kutumia sehemu ya muda wao kuzungumza na watoto na vijana.

Alisema hatua hiyo itasaidia sana kupunguza na kukomesha vitendo vya ukiukaji wa maadili vinavyoendelea kufanywa na baadhi ya watu nchini.

Kwa mujibu wa Mtatiro, vijana wakifundishwa vizuri mila, desturi na kushika mafundisho ya dini na wakawa nahofu ya Mwenyezi Mungu, maovu mengi, zikiwamo ndoa za jinsia moja, ulawiti na unyanyasaji wa kijinsia vitapungua kwa kiwango kikubwa.

Aliongeza kuwa serikali itaendelea kushirikiana na dini zote katika kujenga maadili mema kuanzia ngazi ya familia na jamii kwa ujumla huku akiwaomba viongozi hao kuliombea Taifa na Rais Samia Suluhu Hassan, ili aweze kutekeleza vyema mipango ya maendeleo katika nchi yetu.

Mtatiro alitumia nafasi hiyo kukemea vitendo vya ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto wa kike na wa kiume na kuahidi kwamba serikali ya wilaya itahakikisha inaongeza nguvu katika kupambana na ukatili na kuimarisha ulinzi kwa watoto hao.

Aliwakumbusha viongozi wa dini wilayani humo, kuendelea kukemea vitendo vyote vinavyoweza kuwagawa Watanzania ikiwemo tofauti za dini kwa kuwa sisi sote ni wamoja na kuwapongeza viongozi hao kwa kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano.

Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya BAKWATA Wilaya ya Tunduru, Abdalla Kawanga, aliishukuru serikali kwa kuendelea kushirikiana na viongozi wa dini hali iliyowezesha wilaya kuwa na utulivu na wananchi kupata muda wa kufanya shughuli za uzalishaji mali.


NORWEGIAN CHURCH AID
actalliance

## TAARIFA KWA UMMA

Norwegian Church Aid Tanzania inatoa taarifa kwa Umma ya kuwa imepokea Ruzuku kutoka kwa Wakala wa Norway wa Maendeleo na Mashirikiano(NORAD) kwa ajili ya Usalama wa Chakula na kupunguza njaa. Kwa maelezo zaidi soma hapa chini.

**"JINA LA MRADI: MRADI WA USALAMA WA CHAKULA NA KUPUNGUZA NJAA (Food Security and Reduction of Hunger)–NANSEN Project**

**JINA LA SHIRIKA: NORWEGIAN CHURCH AID (NCA)**

**SARAFU YA BAJETI: KRONA YA NORWAY"**

217535202

| | |
|---|---|
| **Mfadhili** | Wakala wa Norway wa Maendeleo na Mashirikiano - NORAD |
| **Sarafu ya mfadhili** | Krona ya Norway (NOK) |
| **Kiasi cha Ruzuku** | 10,000,000 |
| **Muda** | Miezi 12 |
| **Kipindi cha utekelezaji** | Julai 01, 2023 hadi Juni 31, 2024 |
| **Matokeo ya muda mrefu** | Wanawake, wanaume na vijana wazalishaji wadogo na watoa huduma wamewezeshwa kiuchumi |
| **Matokeo ya muda mfupi** | 1.1 Wazalishaji wadogo wa chakula wameongeza uwezo wa uzalishaji<br>1.2 Wazalishaji wadogo wa chakula kuongeza kipato kupitia shughuli za kuongeza thamani<br>1.3 Wazalishaji wadogo wa chakula wamepunguza upotevu wa chakula kutokana na uzalishaji na usimamizi bora baada ya kuvuna<br>1.4 Kaya zimeongeza upatikanaji wa chakula salama, chenye lishe bora |
| **Wanufaika wa Mradi** | Wanufaika 6,000 wa moja kwa moja, na 30,000 wasio wa moja kwa moja |
| **Mkoa (Wilaya) mradi unakotekelezwa** | Kigoma (Kakonko, Kasulu na Kibondo), Shinyanga (Shinyanga Vijijini na Kishapu), Mtwara (Mtwara DC), Lindi (Mtama, Kilwa), Zanzibar (Pemba), Morogoro (Mvomero, Gairo), Pwani (Chalinze) Kilimanjaro (Moshi Vijijini, Hai na Moshi), Manyara (Babati na Mbulu) na Arusha (Karatu, Arumeru) |
| **Kwa Maelezo Zaidi wasiliana na** | **Mkurugenzi Mkuu<br>Norwegian Church Aid Tanzania (NCA Tanzania)<br>Ploti 436, Barabara ya Mwai Kibaki, Jengo la TCRS ghorofa ya 3<br>S.L.P 3955, Dar Es Salaam<br>Simu: +255 787 770 811 na +255 22 2700252** |

# Wanasheria: Rukhsa mjadala mkataba wa DP World

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya mjadala wa makubaliano ya uwekezaji bandarini baina ya Serikali ya Tanzania na Dubai kupitia kampuni ya DP World, kuendelea kutikisa kwenye majukwaa ya kisiasa nchini, baadhi ya wanasheria wamesema licha ya kuwapo kwa kesi mahakamani, hakuna tatizo kuendelea kuzungumza kutokana na umuhimu wake.

Hoja hiyo inatokana na shauri linapokuwa mahakamani hairuhusiwi kujadiliwa nje ili kuepusha kuingilia uhuru wa mahakama kwa mujibu wa sheria.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wanasheria walisema hakuna kosa kisheria kwa mjadala kuendelea kwenye majukwaa ya kisiasa.

Kesi ya kupinga uboreshaji wa Bandari imefunguliwa katika mahakama ya Mbeya na walifungua ni Watanzania wanne kutoka mikoa mbalimbali.

Walifungua kesi hiyo kupinga baadhi ya vifungu na vipengele vya mkataba huo wa uboreshaji Bandari Tanzania kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai kupitia kampuni ya DP World.

Kesi hiyo namba 05/2023 inamuhusisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Katibu wa Bunge.

Pia, waliofungua kesi wanadai kuwa mchakato wa kuridhia Bunge ni batili kwa kuwa haukufuata utaratibu wa kisheria na bila kuwapa nafasi ya kutosha wananchi kutoa maoni yao kama sheria za nchi zinavyoelekeza.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa rasmi Julai 26, mwaka huu, siku moja baada ya mawakili wa pande zote kuandaa na kuwasilisha mahakamani hoja za msingi walizokubaliana kuwa ndizo zinazobishaniwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema mjadala unaoendelea kuhusu mkataba huo una maslahi mapana ya taifa, na kwamba siyo kosa kuujadili kwa kuwa hauingilii ushahidi au kutoa mwelekeo wa kesi.

"Kesi iliyofunguliwa ni ya madai na ni ambayo ina 'public interest' (utashi wa kijamii) ambayo mara nyingi ni ngumu kuzuia watu kuongea, kwa sababu taifa zima lina 'interest' nalo," alisema Henga.

"Lakini hata hao wanaozungumza kwenye mikutano kwa wananchi, hawazungumzii 'content' (maudhui) za kesi, wao wanaongea suala zima la mkataba, kwa hiyo kesi za namna hiyo mara nyingi unaweza kujadili maadamu haujadili ushahidi ulioletwa mahakamani wala hau-pre-empty (hauiingilii) mahakama kutoa maamuzi kusema nani ana haki na nani hana haki."

"Kwa mfano kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, watu walikuwa wanazungumza pia kwa sababu ya unyeti wa suala lenyewe, na kwa sababu suala la Bandari linaendelea kujadiliwa kama taifa, kuna wanaosema mkataba ni mzuri na wengine wanasema hapana, hivyo siyo mjadala mbaya na hauwezi kuathiri kesi."

Wakili, Jebra Kambole, alisema mjadala huo unaoendelea siyo kosa kisheria.

"Maana wao wanatoa mawazo yao juu ya mkataba na ikumbukwe kwamba mahakama itaamua kutokana na ushahidi na hoja zilizopo mezani sio za magazetini au jukwaani," alisema Kambole.

"Wangekuwa wanafanya makosa kama wangekuwa wamezuiwa na mahakama, lakini wakaamua kuendelea. Kwa kuwa hawawasemi majaji wala hawasemi ni lazima mahakama iamue upande gani, siyo kosa."



Maofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wakiwapa maelezo wanafunzi wa Shule ya Msingi Hijra, wakati walipotembelea banda la tume katika maonyesho ya wakulima Nane Nane Kanda ya Kati katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: MROKI MROKI**

## Kesi kocha wa Simba yapigwa kalenda tena

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya kusafirisha kilogramu 34.89 za dawa za kulevya aina ya heroin, inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Simba, Muharami Sultani na wenzake, imeendelea kupigwa kalenda kutokana na upelelezi kutokamilishwa.

Shauri hilo lilikuja jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Evodia Kyaruzi.

Wakili wa Serikali Erick Kamala akiiwakilisha Jamhuri alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na wanasubiri ripoti mbili kutoka kampuni mbili za simu.

Baada ya kutoa taarifa hiyo, Wakili Kamala aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa ambapo mahakama ilikubali na kuahirisha hadi Agosti 18 mwaka huu.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mmiliki wa Kituo cha Cambiasso Sports Academy kilichoko Tuangoma Kigamboni, Kambi Seif.

Wengine ni Maulid Zungu maarufu Mbonde, Said Abeid, fundi selemala, John Andrew maarufu Chipanda, mfanyakazi wa Kituo cha Cambiasso na Sara Joseph.

Washtakiwa wanadaiwa kuwa Oktoba 27, 2022, huko Kivule, wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kilogramu 27.10.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kuwa Novemba 4 2022, eneo la Kamegele, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, kwa pamoja walikutwa wakisafirisha kilogramu 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroin.

# Upatikanaji dawa Muhimbili wafikia 97%

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili na Amana zimesema upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa sasa ni asilimia 97.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam Mfamasia wa Hospitali ya Muhimbili, Nelson Faustine amesema, hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika taasisi hiyo imeimarika na wameshuhudia mabadiliko makubwa yaliyofanyiwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Tumetoka asilimia 30 hadi zaidi ya asilimia 97 upatikanaji wa dawa katika hospitali yetu ya Muhimbili Upanga na Mloganzila ni hatua kubwa idadi ya wagonjwa imeongezeka kulingana na bajeti, kwa sasa manunuzi yetu ya dawa kwa MSD ni zaidi ya Shilingi bilioni sita kwa mwezi na kwa mwaka ni zaidi ya Sh. bilioni 24," alisema.

Alitoa wito kwa serikali kuongezea mtaji MSD kama ilivyoahidi na kufuta madeni ya nyuma ili kuwezesha taasisi hiyo kujiendesha.

Nelson aliitaka taasisi hiyo ikiwa ni kati ya wateja wakubwa kwa MSD wanapata huduma kwa kipaumbele cha pekee.

Kadhalika, wameitaka MSD kuboresha huduma Muhimbili hususani huduma za kibobezi kuendana na mahitaji ya dawa na vifaa tiba vyake kama vya kupandikiza figo, uboho na uroto ambapo chupa moja ndogo ya dawa hizo ni hadi Shilingi milioni tatu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa Amana, Dk. Brayson Kiwelu, alisema mafanikio makubwa yaliyopo yamechagizwa na Rais Dk. Samia kutokana na maboresho aliyoyafanya sekta ya afya.

"Amana imeweza kupata zaidi ya Shilingi bilioni tano ambazo zimewekezwa katika jengo la kisasa la Ct Scan, X-ray, jengo la dharura, ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi na maboresho kitengo cha usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo.

"Ukarabati huu umeendana na uwekezaji wa vifaa ambapo asilimia 70 ni kutoka MSD, tunajivunia hali ya utoaji huduma na upatikanaji wa dawa ni zaidi ya asilimia 97 changamoto ni dawa za wagonjwa wa saratani, hata hivyo tuna kifungu cha bajeti ya dharura tunazonunua dawa ambazo hazipo," alisema.

# MATANGAZO

TOL Gases Limited
We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## BOARD MEMBER VACANCY.

TOL Gases Limited is the leading manufacturer and distributor of Industrial and Medical Gases. Additionally the Company distributes high quality brands of welding and related consumables as well as medical oxygen related appliances within Tanzania and the neighbouring countries through distributorship arrangements.

The secretariat of the Board of Directors of TOL Gases Limited, do hereby invite shareholders to nominate suitable candidates to be elected to fill **one vacant position of Board Membership. Female Nominees are strongly encouraged.**

**Requirements:**

1. Expertise/Skills in Governance, Risk, Compliance and Administration.

2. Applicants are required to be nominated / proposed by a Shareholder who is duly qualified to be present and vote at the meeting and has signed the proposition to concede his/her willingness to be elected.

3. Any shareholder who would like to nominate / propose a person for election to fill the Board Membership position, may submit the following to the Secretary not later than 20th August 2023 :-
    - Notice of his/her intention to propose such a person signed by the proposed person conceding his willingness to be elected.
    - Resume of the proposed person with due consideration to the requirements of the Companies Act and the Company's MEMARTS.

4. Submission should be delivered to the following address.

**Company Secretary**
**TOL Gases Limited**
**Plot 4b, Nyerere Road**
**P. O. Box 911,**
**Dar es Salaam**
**Email: nlulu@tol-gases.co.tz**
**mjuliana@tol-gases.co.tz**

217535002

Directors: S. Mponji – (Tanzanian) – Chairman, J. Massawe – (Tanzanian), S. Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.C. Kitoka – (Tanzanian).

TOL Gases Limited
We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## NOTICE

## 28TH ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the 28th Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 25thAugust, 2023 at 9.00a.m to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2021 Annual General Meeting held on 19th August, 2022.
3. Matters arising from minutes of the year 2021 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December, 31, 2022.
6. To approve Dividend Payment.
7. To approve Directors' Fees.
8. To appoint Auditors for the year 2023.
9. Election of Directors.
10. To set the place, date and venue of the next meeting.
11. Any other business (Duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no **0685750201/0685750203.**

member entitled to attend and vote at the Meeting is also entitled to appoint a proxy (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his/her stead.

All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz/nlulu@tol-gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**CORNELIUS KASIYA KARIWA**
**COMPANY SECRETARY**

217535002

Directors: S. Mponji – (Tanzanian) – Chairman, J. Massawe – (Tanzanian), S. Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof. A. Temu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian), L.C. Kitoka – (Tanzanian).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upatikanaji dawa hospitalini uendane na ubora wa huduma

**HABARI** njema kwamba Hospitali ya Taifa Muhimbili na Amana sasa zinapata dawa na vifaa tiba kwa asilimia 97.

Hiyo ni hatua kubwa, kwa sababu itapunguza usumbufu kwa wagonjwa wanapokwenda hospitali kupata matibabu na wanapoandikiwa dawa kuambiwa wakanunue maduka ya dawa badala ya kupewa hospitalini.

Sababu ni kwamba baadhi ya dawa kukosekana hospitalini na kupatikana katika maduka ya dawa nje ya hospitali.

Na kwa uzoefu dawa zinazouzwa kwenye maduka ya dawa gharama huwa kubwa kulinganisha na zinazotolewa hospitali na kuwaumiza watu wasiokuwa na uwezo.

Hospitali ya Taifa Muhimbili ni tegemeo la Watanzania wengi wanapopata rufani kutoka kwenye hospitali za chini. Wanapofika hapo na kuambiwa baadhi ya dawa zinakosekana huleta usumbufu kwa wagonjwa.

Ndiyo maana tunasema habari kwamba upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali hiyo imefikia asilimia 97 ni njema na zinaongeza matumaini kwa Watanzania kupata matibabu ya uhakika.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam Mfamasia wa Hospitali ya Muhimbili, Nelson Faustine amesema, hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika taasisi hiyo imeimarika na wameshuhudia mabadiliko makubwa yaliyofanyiwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan.

Hospitali hiyo imetoka kwenye asilimia 30 hadi zaidi ya asilimia 97 ya upatikanaji wa dawa kuanzia Hospitali ya Muhimbili Upanga na Mloganzila na ni hatua kubwa idadi ya wagonjwa imeongezeka kulingana na bajeti, ambapo kwa sasa ununuzi wa dawa hizo kutoka Bohari ya Dawa (MSD) ni zaidi ya Shilingi bilioni 6 kwa mwezi na kwa mwaka ni zaidi ya Shilingi bilioni 24.

Hata hivyo, serikali imetakiwa kuhakikisha inaiongezea mtaji MSD kama ilivyoahidi na kufuta madeni ya nyuma, ili kuwezesha taasisi hiyo kujiendesha.

Hospitali ya Muhimbili ni kati ya taasisi ambazo ni wateja wakubwa kwa MSD na wanapata huduma kwa kipaumbele cha pekee.

Halikadhalika, Bohari ya Dawa imetakiwa kuboresha huduma Muhimbili hususani huduma za kibobezi kuendana na mahitaji ya dawa na vifaa tiba vyake kama vya kupandikiza figo, uboho na uroto ambao chupa moja ndogo ya dawa hizo ni hadi Shilingi milioni tatu.

Vile vile, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa Amana Dk. Brayson Kiwelu amepongeza mafanikio makubwa yaliyopo ambayo yamechagizwa na Rais Dk. Samia kutokana na maboresho aliyoyafanya sekta ya afya.


Hospitali hiyo ya Amana imepata zaidi ya Shilingi bilioni 5 ambazo zimewekezwa katika jengo la kisasa la Ct Scan, X ray, jengo la dharula, ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi na maboresho kitengo cha usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo.

Ukarabati huo umeendana na uwekezaji wa vifaa ambavyo asilimia 70 ni kutoka MSD na hospitali hiyo inajivunia hali ya utoaji huduma na upatikanaji wa dawa ambao ni zaidi ya asilimia 97.

Changamoto ni dawa za wagonjwa wa saratani ambazo hata hivyo limetengewa kifungu cha bajeti ya dharura kinachonunua dawa zinazokosekana.

Tunasema ni hatua kubwa na Watanzania wanatarajia huduma bora zaidi katika hospitali hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuchangie damu kuokoa wengine

**WATANZANIA** wanaopoteza maisha kwa kukosa damu, inaumiza sana kufiwa na ndugu tena inauma zaidi kwa kukosa damu, ambayo kila mmoja anayo na anaweza kuitoa kunusuru maisha.

Watu wanashindwa kuchangia damu ilihali afya zao ni imara na hali inaruhusu tena na hakuna madhara watakayopata wakichangia damu.

Wajawazito, wazazi, watoto wachanga, majeruhi wa ajali, wagonjwa wa maradhi sugu kama saratani wote wanahitaji damu na kama ikikosekana wengine hupoteza maisha.

Wodi ya wazazi inahitaji huduma hiyo kuokoa wazazi na watoto wachanga ambao wakikosa damu wakati mwingine wanaweza kufa pamoja na watoto wachanga.

Endapo utampoteza jamaa yako kuanzia mzazi, majeruhi na hata mtoto mchanga na ukaelezwa kuwa sababau ya kifo ni kukosa damu au chembe hai nyeupe maneno haya unapopewa na daktari kama ndio sababu ya kifo cha ndugu yako yanakuumiza sana.

Jamii inapaswa kujenga utaratibu wa kuchangia damu ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu ambao wanakumbana na changamoto za kuishiwa au kupungukiwa.

Ipo haja ya kuiunga mkono juhudi za serikali na Wizara ya Afya ili kukabiliana na uhaba wa damu ulioko katika hospitali mbalimbali nchini.

Licha ya nadharia kwamba mtu hawezi kulazimishwa kuchangia damu lakini kuna faida kadhaa unapotoa damu ili kuokoa uhai wa binadamu wenzako,

Hii ni pamoja na kutoa sadaka iliyo hai, pia kuwa mwanachama wa kudumu kwenye regista ya watoa damu na taarifa zako zinarekodiwa kwamba uliwahi kuchangia damu na kuokoa maisha ya wengine. Damu ya binadamu hakuna mahali pengine inapatikana au inauzwa zaidi ya kwenye mwili wa wake, haipandwi hata hailimwi shambani kama mahindi, hapa panahitajika moyo wa mtu anayeumia kwa kuona mwenzake anapoteza maisha kwa kukosa damu na hivyo kuamua kuchangia kwa hiari.

Hivi karibuni Kikundi cha Daraja Salama kinachoundwa na wanafamilia wanaotoka mikoa mbalimbali waliojiunga pamoja kutoa huduma za jamii kama kuchangia damu, kusaidia yatima na wajane walifika katika Hospitali ya Rufani ya Temeke, Dar es Salaam kutoa huduma hiyo. Juhudi zao zinaungwa mkono na wananchi majirani wa hospitali ya Temeke wanaojitokeza kusaidia wagonjwa wenye shida ya damu.

Akiwashukuru na kuwapongeza Juhudi Nyambuka daktari wa afya, wa hospitali hiyo anaeleza kuwa ukosefu wa damu unasababisha watu kupoteza maisha.

Akizungumzia sababu za kuogopa kutoa damu Juhudi, anasema wapo wanaohofia kuchunguzwa VVU na UKIMWI bila kufahamu kwamba hakuna atakaye lazimishwa kupima, damu ndiyo itakayopimwa na majibu itabaki siri ya daktari.

Anasema hakuna sababu ya kuogopa kuchangia damu akieleza kuwa iwapo kutakuwa na banki yenye damu ya kukidhi mahitaji kuna uwezekano mkubwa wa kuepuka vifo vinavyotokana na uhaba huo.

Anaeleza kuwa ukifika hospitalini kama una nia ya kuchangia damu utapewa kipaumbele na milango ipo wazi kila siku kwa kuwa wanajua umuhimu wa damu kwa wagonjwa wenye upungufu.

Anakiri kuwa bado kuna shida, kuelewa umuhimu wa kuchangia damu hasa maeneno ya vijijini na elimu na uhamasishaji vinahitajika.

Katika eneo hilo anaitaka serikali kuongeza nguvu zaidi kwa ajili ya kutembelea vijiji mbalimbali kama viwandani, ofisi za umma na binafsi,taasisi za elimu kama sekondari na vyuo vya kati na vikuu, kuhamasisha watu kuchangia damu.

Nina amini juhudi hizo zikifanyika kwa mikakati na mipango bora ipo siku, uhaba wa damu utakuwa siyo tatizo kubwa katika nchi yetu kama ilivyosasa na hivyo kunusuru maisha ya wazazi, majeruhi, watoto na wanaoteseka na magonjwa ya kusendeka.

HABARI KITAIFA

# Mpango apongeza utoaji elimu ya fedha, mikopo kwa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amezitaka taasisi za fedha nchini kutumia vyema maonyesho ya kilimo ya NaneNane yanayoendelea jijini Mbeya kwa kutoa elimu kuhusu masuala ya fedha kwa wakulima.

Dk. Mpango pia ameipongeza Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa kuandaaa banda maalumu kwa ajili ya kutoa elimu hiyo kwa kundi hilo.

Kiongozi huyo wa serikali alitoa rai hiyo juzi baada ya kutembelea banda la maonyesho hayo la Benki ya NBC kwenye uwanja wa John Mwakangale jijini hapa, akifuatana na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na viongozi wengine waandamizi serikalini.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango hatua hiyo itawasaidia wakulima kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya kifedha ikiwamo aina ya mikopo inayotolewa na taasisi hizo, viwango vya riba na makato mengine ili wafanye uamuzi sahihi pindi wanapofanya uamuzi mbalimbali unaohusisha fedha.

"Nimevutiwa zaidi kuona Benki ya NBC katika suala hili la elimu ya fedha mmeliwekea msisitizo mkubwa kiasi kwamba mmetenga eneo maalumu kwa ajili ya utoaji wa elimu kuhusu huduma zenu za kifedha hususani riba na uwekezaji kwa wakulima... hongereni sana kwa hatua hii."

"Ningependa taasisi zingine zifanye hivyo pia. Ninatamani kuona taasisi za fedha zinatumia vyema maonyesho haya kwa faida ya wakulima si tu kutoa huduma zao kwa washiriki bali pia elimu ndiyo iwe kipaumbele," aliagiza.

Akifafanua kuhusu baadhi ya huduma za benki hiyo mahususi kwa wakulima, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na Wakulima NBC, Raymond Urassa, alisema benki hiyo imeendelea kubuni huduma zaidi mahususi kwa wakulima ikiwamo mikopo ya zana za kilimo (matrekta, mashine za kuvuna), huduma za bima ya kilimo, programu maalumu ya utoaji wa elimu ya fedha kwa wakulima sambamba na kuwaunganisha wakulima na mitandao ya kibenki ili kuwarahishia huduma za kibenki.

"Kwa mwaka huu pekee tayari tumetoa mikopo ya matrekta 69 kwa wakulima ili kuongeza matumizi ya vifaa vya kisasa katika sekta kilimo. Kupitia huduma ya bima, kwa kushirikiana na kampuni ya bima ya Jubelee tunatarajia kuwalipa fidia wakulima wa tumbaku walioathirika na mvua za mawe katika msimu wa kilimo mwaka jana," alisema Urassa.

Akizumzungumzia zaidi kuhusu elimu ya fedha kwa wakulima, Urassa alimhakikisha Dk. Mpango kuwa benki hiyo inayatumia vyema maonyesho hayo kwa kuhakikisha kuwa mbali na kutoa huduma za kifedha kwa washiriki, pia msisitizo unawekwa katika utoaji wa elimu kwa wakulima wakubwa na wadogo ili waelewe vizuri huduma za benki hiyo, aina ya mikopo inayotolewa na riba zake pamoja na elimu ya uwekezaji katika fursa mbalimbali za sekta ya kilimo.

"Tulibaini kuwa wakulima wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu riba na viwango vyake. Kwahiyo, walikuwa wanakopa bila kujua tafsiri ya viwango vya riba, jambo ambalo ni muhimu sana na hiyo ndio sababu kupitia maonyesho haya elimu ya mambo kama hayo tumeipa kipaumbele," alisema.

Alitoa wito kwa wakulima na wadau wengine wa kilimo na washiriki mbalimbali wa maonyesho hayo kutembelea banda la benki hiyo ili kunufaika na elimu inayotolewa bila malipo kuhusu huduma mbalimbali za kifedha zinazohusiana na sekta ya kilimo, huku akiahidi kwa niaba ya benki hiyo kuendelea kubuni na kutoa huduma zinazoendana na mahitaji wa wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo wakiwamo wakulima wakubwa na wadogo, wasambazaji wa pembejeo za kilimo pamoja na wauzaji mazao ya kilimo.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo, Lariba na wakulima wa Benki ya NBC, Raymond Urassa (kulia), kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo kwa wakulima alipotembelea maonyesho ya kilimo Nanenane katika viwanja wa John Mwakangale, mkoani Mbeya juzi. Wengine ni Spika Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto) na Meneja wa benki hiyo Tawi la Mbeya, Asia Mselemu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upelelezi wakamilika kesi ya mashtaka 143 watumishi jiji

**Na Kulwa Mzee**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili watumishi wa jiji la Dar es Salaam, Tulusubya Kamalamo na wenzake, umedai upelelezi umekamilika.

Wakili wa serikali, Yusuph Aboud, akisaidiana na Titus Aron, alidai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo, wakati kesi hiyo ilipokuwa inatajwa jana.

Watumishi hao wa jiji wanakabiliwa na mashtaka 143, likiwamo la kughushi na kulisababishia hasara jiji hilo zaidi ya Sh. bilioni 8.9.

Wakili Aboud alidai upelelezi wa shauri hilo tayari umekamilika na wako katika hatua ya kuandaa taarifa muhimu wazipeleke mahakama kuu.

Upande wa Jamhuri uliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo na mahakama ilikubali, ikapanga Agosti 14 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Katika hatua nyingine, washtakiwa hao waliondolewa shtaka la utakatishaji fedha isipokuwa mshtakiwa Said Bakari. Mahakama iliwaelekeza washtakiwa ambao wamefutiwa shtaka la utakatishaji fedha kuwasilisha maombi ya dhamana mahakama kuu kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi yao.

Washtakiwa wengine ni pamoja na James Bangi (mhazini), Mohamed Khars, Abdallah Mlwale, Alinanuswe Obel na Deogratias Lutatuza ambao ni wahasibu na Judica Ngowo (karani wa fedha).

Wengine ni Febronia Nagwa, Glory Eugen, Said Bakari, Josephine Sandewa, Dorica Gwihala, Jesca Lugonzibwa, Patrick Chibwana (wote wahasibu), Patrick Chubwana (Ofisa Afya), Ally Baruan (meneja) na Khalid Nyakamande (Ofisa Mtendaji wa Mtaa).

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Julai Mosi 2019 hadi Juni 30, 2021, washtakiwa hao kwa pamoja waliongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. 8,931,598,500 (bilioni 8.93/-) mali ya Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam.

Washtakiwa wanadaiwa kutumia madaraka yao vibaya kwa kushindwa kuingiza malipo ya watu mbalimbali katika akaunti za jiji hilo zilizoko katika benki za NMB, NBC, CRDB na DCB.

Mshtakiwa Judica, Febronia, Bakari na Glory wanakabiliwa na mashtaka 53 ya kuingiza taarifa za udanganyifu katika mfumo wa malipo kwa lengo la kuonyesha malipo ya watu mbalimbali yaliingizwa katika akaunti za jiji hilo wakati wakijua si kweli.

Inadaiwa washtakiwa hao isipokuwa Dorica, Chibwana, Baruani na Nyakamande, wakiwa wahasibu, pia wahazini, wanakabiliwa na mashtaka ya ubadhilifu wa Sh. 8, 931, 585,500 kwa kuzitumia kwa matumizi yao binafsi.

Pia inadaiwa katika tarehe hizo, washtakiwa Kamalamo, Bangu, Sandewa, Gwihala, Lugonzibwa, Chibwana, Baruan Alinanuswe na Nyakamande walighushi nyaraka mbalimbali zionekane ni halisi wakati wakijua si kweli.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# Dada wa kazi kizimbani mashtaka kuingilia mfumo na kuiba Mil. 13.8/-

**Na Grace Gurisha**

MFANYAKAZI wa ndani, Riziki Kanena (22), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, akikabiliwa na mashtaka matano, likiwamo la kuingilia mfumo wa kompyuta na kujipatia Sh. 13,800,000.

Mbali na Kanena mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Laulentina Yustad (43), anayekabiliwa na shitaka la kupokea fedha kutoka kwa mshtakiwa Riziki.

Wakili wa Serikali, Titus Aron alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Pamela Mazengo wakati akiwasomea mashtaka yao kwa mara ya kwanza katika mahakama hiyo.

Aron alidai kuwa kati ya Januari 3, 2023 na Juni 5, 2023, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam, kwa makusudi na kinyume cha sheria, mshtakiwa aliingilia mfumo wa kompyuta kwa kutumia huduma ya benki mtandao ya CRDB.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 3, 2023 na Juni 5, 2023, huko Mikocheni, ndani ya Wilaya ya Kinondoni, mshtakiwa alifanya udanganyifu kwa njia ya kompyuta na kujipatia Sh. 13,800,000.

Aron alidai kuwa katika shtaka la tatu inadaiwa kuwa tarehe hiyo na eneo hilo, mshtakiwa aliiba fedha hizo ambazo ni mali ya Florence Kazimoto kupitia huduma hiyo ya benki huku akijua kufanya hivyo ni kosa.

Katika shtaka la tatu, kati ya Januari 3 na Juni 2023, katika Mtaa wa Akamea Karagwe, Kijiji cha Mlamba, mkoani Kagera kupitia namba yake ya simu, mshtakiwa wa pili Yustad alipokea Sh. 5,423,000 huku akijua kuwa zilipatikana kwa njia isiyo halali.

Alidai kuwa katika shtaka la tano kati ya Januari 3, 2023 na Juni, 2023, Mikocheni, Dar es Salaam, Riziki alitumia laini ya simu ya mtu mwingine iliyosajiliwa kwa jina la Yusuph Anthoni Mboko bila kumjulisha mhusika.

Mshitakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Agosti 14, 2023, kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.



Mratibu wa Mama na Mtoto wa Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, Caroline Maliseli (kulia), akieleza namna mabinti balehe wanavyopata ujauzito wakiwa na umri mdogo chini ya miaka 20 katika kikao cha majadiliano ya kupambana na vitendo vya kikatili wa kijinsia kwa wanawake, watoto na kundi la wazee kilichoandaliwa na HelpaAge International Tanzania, wilayani Kahama jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## UFADHILI WA MASOMO

# OUT waja na programu maalumu, wahitimu wenye ufaulu mdogo

**Na Miraji Msala**

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kimeandaa programu maalumu ya mafunzo kwa wanafunzi wa kike waliohitimu kidato cha sita katika masomo ya sayansi na ufaulu wa angalau E na S katika masomo mawili ya tahasusi zao.

Dk. Mohamed Maguo, Mhadhiri Mwandamizi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Masoko wa OUT, alibainisha mkakati huo jana jijini Dar es Salaam.

Alizitaja tahasusi zinazolengwa ni PCM, PCB, CBG, PGM, CBA na EGM. Pia, wahitimu wa diploma wenye ufaulu wa GPA 2.9-2.0 na wenye 'NTA level 5/Professional Technician level II Certificate'.

Dk. Maguo alisema wahitimu wenye sifa hizo watajiunga na programu hiyo. Watapata mafunzo ya kina kwa ana kwa ana pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa kipindi cha miezi mitatu.

"Wahitimu hawa ni wale ambao wanaotokea katika familia zenye changamoto mbalimbali kama vile wanaotoka maeneo ya pembezoni, familia maskini, wenye ulemavu na yatima.

"Hawa watapewa kipaumbele. Sababu hizi zimepelekea wanafunzi hawa kutopata sifa za moja kwa moja kujiunga na elimu ya juu. Mradi huu pia unalenga kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike katika elimu ya juu katika fani za sayansi, teknolojia, uhandisi na afya," alifafanua.

Alisema ufadhili wa masomo hayo yatatolewa kwa asilimia 100 na Serikali ya Tanzania. Utajumuisha ada na gharama zingine za mwanafunzi na chuo.

Jinsi ya kutuma maombi, Dk. Maguo alisema waombaji wanaweza kufika katika vituo vya OUT ambavyo vipo katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar; Unguja na Pemba. Pia, wanaweza kupata fomu katika tovuti ya chuo kikuu hicho na kuzijaza na kuzituma.

Alisema maombi yatapokelewa mpaka tarehe 5 Agosti mwaka huu ambayo itakuwa ndiyo siku ya mwisho ya kupokea maombi.

"Wahitimu watakaomaliza programu hii watapata sifa ya kujiunga na shahada ya kwanza katika vyuo mbalimbali nchini.

"Wahitimu hao watapata fursa ya kuomba mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu wakiwa katika masomo yao ya shahada.

"Mradi huu ni wa miaka mitano na utahusisha ufadhili wa wanafunzi 1,000. Kila mwaka watafadhiliwa wanafunzi 200. Huu ni ufadhili kwa wahitimu wa kike kwa asilimia 100 kama ilivyoelezwa hapo awali," alisema.

Alifafanua kuwa wanafunzi ambao hawatofaulu au kutimiza vigezo wataendelea na masomo kwa njia za kawaida na kufanya mitihani ya marudio. Watakaoshindwa mitihani ya majaribio, ufadhili utasitishwa.

Aliishukuru serikali kupitia Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi huo kwa lengo la kuwaendeleza watoto wa kike katika masomo ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya Taifa.

# Stanbic yatwaa tuzo ya Benki Bora ya Uwekezaji

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Stanbic Tanzania imetambuliwa kama Benki bora ya uwekezaji Tanzania kwa mwaka wa pili mfululizo katika tuzo za Euromoney 2023.

Euromoney imekuwa ikitathmini taasisi za fedha zinazoongoza duniani kupitia taarifa za utendaji, utafiti, na tuzo za sekta kwa zaidi ya miaka 30. Programu yao ya tuzo za kila mwaka inatambua ufanisi katika makundi ya kimataifa, kikanda na ya nchi moja moja.

"Ni heshima kwetu kutambuliwa tena kama Benki bora ya uwekezaji Tanzania na Euromoney mwaka 2023. Ushindi huu unaonesha dhamira yetu ya kutoa suluhisho zinazochochea ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kuthibitisha kusudi letu, Tanzania ni nyumbani kwetu, tunachochea ukuaji wake." Alisema Manzi Rwegasira, Kaimu Mtendaji Mkuu na Mkuu wa Idara ya Uwekezaji na Biashara katika Benki ya Stanbic.

"Kutambuliwa na moja ya machapisho ya fedha yanayoaminika zaidi duniani kuna onyesha tumefikia kiwango cha ufanisi katika kuongeza thamani kwa wateja na nchi kwa ujumla," alisema.

Alisema kuwa kama sehemu ya Standard Bank Group, benki kubwa zaidi barani Afrika kwa mali/dhima, na uwakilishi katika nchi zaidi ya 20 za Afrika, na masoko muhimu ya kifedha, idara ya uwekezaji na biashara ya Benki ya Stanbic inatoa huduma za mikopo kwa kampuni kubwa na miradi mikubwa, ushauri na masoko ya fedha za kigeni.

Elibariki Ndossi, Mkuu wa Uwekezaji wa Benki ya Stanbic Tanzania, alisema: "Wateja ndiyo kipaumbele chetu kwa kila tunachokifanya, na nia yetu ni kuwapa suluhisho zinazotatua mahitaji yao binafsi zinazo wawezesha kufikia malengo yao ya uwekezaji.

"Tofauti kubwa inayotolewa na kitengo cha biashara na uwekezaji cha Benki ya Stanbic ni upatikanaji wa utaalamu wa ndani na wa kikanda kutoka kwa timu ya wataalamu waliobobea katika masuala ya uwekezaji."

Alisema kutambuliwa kwa mafanikio hayo kwa miaka miwili mfululizo ni jambo kubwa linalochochea shauku na ahadi yao kwa wateja na nchi.





# DC ahimiza uhifadhi wa msitu asilia

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI wilayani Same imetoa angalizo kwa wadau wa uhifadhi kutoa kipaumbele cha uanzishwaji wa miradi ya utunzaji wa mazingira itakayosaidia kukuza kipato kwa jamii zinazoishi kandokando ya Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia wa Chome.

Hifadhi hiyo ina ukubwa wa hekta 14 283 na urefu wa mpaka kilometa 67 inazungukwa na vijiji 27, kwenye kata 11 ambazo wakazi wake kwa kiasi kikubwa maisha yao hutegemea uwapo wa hifadhi ya Chome kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Kasilda Mgeni, alisema jana kuwa baada ya kutembelewa na wataalamu wa mazingira wa miradi wa kanda ya kaskazini kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF), wakiambatana na Ofisa misitu kutoka ofisi ya Mkuu Mkoa wa Kilimanjaro, alisema endapo jamii zitawezeshwa kwa kupewa elimu, uharibifu wa mazao ya misitu utapungua.

"Wataalamu hakikisheni mnatoa kipaumbele kwa jamii za kandokando ya hifadhi katika uanzishaji wa miradi ya utunzaji wa mazingira. Hii itawasaidia kuongeza kipato kwa jamii na suala la mirungi litabaki kuwa historia kwa kuwa sasa linaathari kubwa kwa nguvu kazi na kukwamisha maendeleo," alisema.

Ofisa Misitu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Emanuel Kiyengi, alisema hifadhi hiyo ina umuhimu kitaifa na kimataifa kutokana na vyanzo vingi vya maji vilivyoko na utajiri wa bioanuwai ambayo imegawanyika katika maeneo matano ya usimamizi ambayo ni Chome, Suji, Mamba Myamba, Bombo na Bwambo.

"Hifadhi ya mazingira asilia ya chome ni hifadhi yenye umuhimu wa kipekee si tu kwa wakazi wa wilaya ya Same bali pia hata kwa taifa kwa ujumla. Ndege aina ya Ndwele anayeitwa 'South Pare White Eye' anapatikana hapo, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha wanautunza, "alisema.

# Waziri aagiza BRELA kuweka kambi Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, ameiagiza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)kuweka kambi mkoani Arusha kwa ajili ya kurasimisha wafanyabiashara wa kilimo ili wapate leseni, namba za utambulisho wa walipakodi (TIN) na vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi.

Pia amewaagiza wafanyabiashara wazawa kuacha mara moja tabia ya kukata leseni na kuwauzia wageni kutoka nchi ya jirani wanaoingia nchini kununua mazao hadi mashambani badala ya kuyafuata kwenye soko husika.

Dk. Kijaji alitoa maagizo hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mkoani hapa kwa lengo la kujua matatizo yao na serikali ifanyie kazi.

"Endapo wafanyabiashara wa mazao wakirasimishwa na kupata leseni zao, watatambuliwa na serikali kwa kubaini idadi yao na kujua mnyororo wa thamani na kujikwamua kiuchumi.

"Lakini najiuliza inakuwaje kibali cha mazao kuuzwa kwa mtu mwingine tena raia wa nje ya nchi ilhali vibali vinatolewa kwa watanzania wanaouza mazao hayo?

"Hili sitalikubali kwa nini serikali itoe vibali vya mazao kwa wafanyabiashara halafu wafanyabiashara hao hao baadhi wanawauzia wageni kutoka nchi Jirani? Hapa kuna mchezo unaofanyika na nitaongea na Waziri wa Kilimo (Hussein Bashe) ili kudhibiti vibali kwa kuwa ni lazima tuwarasimishe ili tudhibiti haya na mizigo mnayosafirisha nje ya nchi kwa kuwa kila mkifika mpakani na mazao yenu mtapewa risiti. Tunataka tujue mmebakiza tani ngapi maana awali mlituchezea kwa kuvusha mazao kwa kutumia udanganyifu," alisema.

Pia serikali itafuta vibali vya usafirishaji wa mazao vinavyokatwa kila mkoa, badala yake kibali kiwe kimoja tu kilicholipiwa kila kitu ili wafanyabiashara wa mazao wabebe mizigo na kupelekea mahali husika bila kukata vibali kila mkoa wanapopita.

Alitaka wajiandae kutumia mfumo maalum wa kulipia vibali kupitia simu za mikononi (simu janja) kwa kujaza taarifa zao sahihi.

Kuhusu suala la Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa kazi (OSHA), Jeshi la Zimamoto na Ukoaji alisema atakuja na Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi na Waziri wa Kazi, wakiambatana na wataalam wa Idara ya Uhamiaji, ili kujua gharama halisi ya ulipiaji wa hati za kusafiria na kiasi wanachopaswa kutozwa wananchi.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuondoa malalamiko katika idara hizo juu ya ulipwaji wa kodi za upimaji afya kazini na zimamoto na kuhusu gharama halisi ya vifaa vya moto .

Awali, baadhi ya wafanyabiashara, Edward Wilson, Thomas Kirusha na Aminah Njoka,ambaye ni Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wadogo (Machinga) pamoja Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji Mikoa wa Arusha na Kilimanjaro, Locken Adolf, walizilalamikia OSHA, Zimamoto na Uhamiaji kwa kuwatoza fedha tofauti na kodi.

Malalamiko mengine yalielekezwa kwa Halmashauri ya Jiji la Arusha kupitia baadhi ya watumishi kuwasumbua wafanyabiashara kwa kukamata mizigo ya biashara na kufunga maduka.

Wilson aliomba serikali kuwasaidia wafanyabiashara wa mazao ambao kwa sasa mazao yao wanauza kwa bei zisizojulikana kutokana na wafanyabiashara kutoka nchi ya jirani kwenda kwenye mashamba moja kwa moja wakisaidiwa na Watanzania wanaokata vibali vya kusafirisha mazao na kuwauzia hali inayoleta kero sokoni.

Naye Njoka, akizungumza kwa niaba ya wamachinga, alilalamikia wateja kutofika maeneo walitotengewa na serikali kutokana na baadhi kupelekwa kwenye masoko yasiyo rafiki. Aliiomba serikali kujenga masoko ya kisasa jijini Arusha ambayo yatawajumuisha wafanyabiashara wote kuuza bidhaa kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.



Wakazi wa kijiji cha Mmbogo, kata ya Lwande wilayani Kilindi mkoani Tanga, wakikagua shimo kubwa la choo linalochimbwa kwa ajili ya zahanati ya kijiji hicho, baada ya kumalizika kwa mkutano mkuu kuhusu mapato na matumizi kijijini hapo, juzi. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Mwenyekiti CCM ageuka mbogo utekelezaji hafifu mradi maji

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdurahman, ameeleza kutoridhishwa na utekelezaji wa mradi wa maji wilayani Mkinga uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.1.

Kutokana na kutoridhishwa huko, amemtaka Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, na Mkuu wa Mkoa, Waziri Kindamba, kutembelea mradi huo na kuchukua hatua endapo itabainika kuwapo kwa ubadhilifu wa aina yoyote.

Mradi huo unaosimamiwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mkinga, unadaiwa utekelezaji wake hauna ufanisi wala tija kwa wananchi wapatao 10,000 wanaokabiliwa na adha ya maji.

Mwenyekiti huyo aliyasema hayo juzi akiwa wilayani hapa wakati wa mwendekezo wa ziara yake ya kukiimarisha chama na kukagua miradi ya maendeleo.

Pia alisema watendaji watakaobainika kufanya ubadhirifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, wanatakiwa wachukuliwe hatua kali za sheria.

Alisema ni lazima wanyooshane mapema hasa kwa wale watumishi ambao ni wazembe wanashindwa kutekeleza wajibu wao na kusababisha kukipa chama hicho taabu wakati wa kampeni huku akisisitiza kwamba hawatakubaliana na jambo hilo na wataanza kuchukua hatua kabla ya kukutana na maswali kutoka kwa wananchi.

Pia alisema kitendo kilichofanywa na RUWASA Wilaya ya Mkinga cha kujenga tangi la maji kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi bila kuwa na chanzo cha uhakika ni kuichonganisha serikali na wananchi wake.

Alisema alitarajia kuona ujenzi wa tangi hilo la mbali na utekelezaji wa miundombinu ya kupokea maji, kusafirisha na kusambaza maji ungeenda sambamba na ukarabati wa bwawa la maji la Gombero ambalo ndilo chanzo kikuu cha upatikanaji wa huduma hiyo.


Kilichoonekana kwenye mradi huo, alisema tangi la maji liko lakini hakuna uhakika wa upatikanaji wa huduma hiyo na mwisho serikali inamlipa mkandarasi pesa nyingi huku wananchi wakiendelea kuteseka kwa kukosa maji.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wanahangaika mchana na usiku kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo itakayowasaidia wananchi kuondokana na kero mbalimbali lakini cha kusikitisha watendaji walioopewa dhamana hawatekelezi walichoagizwa.

Akitoa ufafanuzi kutokana na madai hayo, Meneja wa RUWASA Wilaya Mkinga, Thomas Kaijage, alisema bwawa hilo lina changamoto na linahitaji kufanyiwa ukarabati lili kutunza maji ya kutosha yatakayohudumia wananchi. Pia alisema wanategemea kupata fedha kwa bajeti ya mwaka 2023/24.

Kaijage alisema kwa mujibu wa mkataba wa utekelezaji wa mradi huo, kazi ya ukarabati wa bwawa hilo itafanywa na Wakala wa Uchimbaji wa Mabwawa na Visima (DDCA) baada ya usanifu kukamilika.

Hata hivyo, alisema mradi unaojengwa wilayani hapa unakwenda sambamba na ujenzi wa tangi la maji litakalokuwa na uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo 300, vituo 28 vya kuchotea maji, ofisi ya chombo cha watoa huduma ngazi ya jamii (CBWSO), machujio ya maji, uchimbaji na ulazaji wa mabomba na ufukuaji wa mitaro mita 48,000 na ukarabati wa nyumba ya pampu.





# 2,600 wajifungua katika umri mdogo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WASICHANA 2,619 wenye umri chini ya miaka 20 katika Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, wametajwa kujifungua katika umri mdogo mwaka 2022, wengi wao wakiwa ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za manispaa hiyo.

Chanzo cha hali hiyo kimeelezwa ni mila na desturi potofu ndani ya jamii ambazo zimekuwa zinahamasisha wanafunzi na watoto kuozeshwa katika umri mdogo, pia vitendo vya ubakaji vinavyofanywa mara kwa mara.

Takwimu hizo zilitolewa juzi na Mratibu wa Mama na Mtoto wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Caroline Maliseli, katika kikao kazi cha kujadili namna ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wazee, kilichoitishwa na HelpAge International Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2022, wajawazito 17,605 walijifungua. Kati yao, 2,619 walikuwa wasichana wenye umri chini ya miaka 20 sawa na asilimia 16.8 na wengi wao ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Alisema tatizo la ndoa za utoto ni kubwa na linapaswa kutafutiwa ufumbuzi ili kuwapatia nafasi watoto wa kike kusoma.

Alisema idadi hiyo ni ya waliofika katika vituo vya afya na kupata huduma huku kundi kubwa likisalia majumbani na kuzalishwa na wakunga wa jadi wasiokuwa wataalamu wa afya.

Alibainisha kuwa wanawake 497 sawa na asilimia tatu walioji-fungulia kwa watoa huduma hao walihatarisha afya zao pamoja na watoto katika mwaka tajwa.

Mratibu huyo alisema kuwa kwa mwaka 2021, kulikuwa na tukio la mjamzito kuzalishwa ndani ya duka la dawa, mtoto alipotanguliza mgongo na miguu, yule muuza dawa alichukua kifaa cha baiskeli na kukitumia kukata kichwa cha mtoto na baada ya tukio hilo alitoweka na mama akabaki anatokwa damu nyingi.

Alieleza kuwa mama alipofikishwa hospitalini na kufanyiwa upasuaji na kuondoa kichwa cha mtoto tumboni, ilibainika kilikuwa kikubwa.

Mama hakujua kwa kuwa hakuwa na mahudhurio ya kliniki kipindi chote cha ujauzito.

Alisema kuwa mama alipona, lakini akapoteza kichanga chake. Akawataka wanawake kuacha tabia hiyo na badala yake wanapopata ujauzito wawe na mahudhurio ya kliniki na kwenda hospitalini au kituo cha afya wanapopata uchungu.

"Ofisini kwangu kuna chupa nyingi za dawa za asili za kuongeza uchungu kwa mjamzito, ninazikamata pale wajawazito wanapofika hospitalini kujifungua, wengi wanapoteza maisha wanapozitumia na kusababisha mfuko wa uzazi kupasuka na mtoto kunywa maji machafu, na yote hayo wanayafanya kwa maelekezo ya mama wakwe zao," alisema Maliseli.

Diwani wa Kagongwa, Ismail Masolwa, alisema shida hiyo inasababishwa na kuwapo imani potofu - mjamzito anapojifungulia nyumbani au kwa mganga wa jadi anakuwa jasiri ndani ya familia. Ni hatari kwa usalama wa mama na kichanga.

Mratibu wa Mradi wa Chaguo Langu Haki Yangu kutoka HelpAge International Tanzania, Joseph Mbasha, alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa miwili ya Shinyanga na Mara kwa lengo la kutokomeza vitendo hivyo.

Alisema mila na desturi potofu ni kikwazo katika kumpatia nafasi mwanamke kushiriki, kujisimamia na kutimiza ndoto zake kulingana na majukumu yake ya kijinsia yanayomhitaji na ndiyo sababu ya kukutana na kujadili namna ya kuzitokomeza.

## 'Viongozi simamieni utekelezaji wa miradi'

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Abdalla Shaib Kaim, amewataka viongozi wa Mkoa wa Shinyanga kuendelea kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aliagiza hayo jana wakati wa makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru kutoka mkoani Shinyanga kwenda Geita.

Alisema ameupongeza Mkoa wa Shinyanga kwa miradi yao mizuri, Mwenge ukipitishwa katika miradi yote 41, Hakuna mradi ambao umekataliwa.

"Ninawasihi viongozi wa Mkoa wa Shinyanga mwendelee kusimamia vizuri miradi yote ya maendeleo ambayo inaendelea kutekelezwa, ili iwe na ubora na thamani ya fedha ionekane," aliagiza Kaim.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema Mwenge huo ukiwa katika Mkoa wa Shinyanga, umekimbizwa umbali wa kilomita 571.5 na kupitia miradi ya maendeleo 41 yenye thamani ya Sh. bilioni 14.2.

Alisema miradi ya maendeleo ambayo imewekewa mawe ya msingi, wataendelea kuisimamia ili itekelezwe kwa kiwango na ubora unaotakiwa. Mwenge wa Uhuru katika Mkoa wa Shinyanga ulianza kukimbizwa Julai 27 mwaka huu. Jana ulikabidhiwa kwa Mkoa wa Geita.




Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella (kulia), akizindua tawi la Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Geita, eneo la soko la dhahabu mkoani Geita mapema wiki hii, ikiwa ni moja ya mipango ya kusogeza huduma za kifedha kwa wananchi. Anayemsaidia ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi kata wapewa angalizo weledi kazini

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, amewataka maofisa polisi wakaguzi wa kata kuwa mfano bora katika kuimarisha ulinzi katika maeneo yao na kuepuka kuwa chanzo cha uvunjifu wa amani na maadili kwa kushirikiana na watu wenye nia ovu.

Amos Makalla alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na maofisa hao, watendaji wa kata na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kikao kazi alichoitisha jijini."Suala la kushirikisha wananchi katika ulinzi na usalama ni muhimu sana. Ninaamini katika utendaji kazi wenu, ninawaombeni mwongeze weledi katika kazi hii kwa maslahi ya wananchi," aliagiza.

Makalla pia aliagiza ushirikiano kati ya jeshi hilo na vyombo vingine ili kuhakikisha uhalifu unadhibitiwa, akiwataka wakaguzi hao kufanya kazi kwa weledi pasi na kumwonea mtu.

Mkuu wa Kamisheni ya Polisi Jamii nchini, Kamishna Faustine Shilogile, aliwataka watendaji wa kata nchini kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi ili kuhakikisha wanatokomeza vitendo vya uhalifu.

"Tunaposema amani na ulinzi shirikishi, kunatakiwa kuwapo na muungano wa nguvu za kiutendaji kutoka kwa watendaji wa kata, mitaa, vijiji pamoja na wananchi, maana wanafahamu maeneo yao ili kuwasaidia polisi jamii katika majukumu yao.

Neema Tashi, mkazi wa Kata ya Mahina, wilayani Nyamagana, alilishukuru jeshi hilo kwa kutambua mchango wa wananchi katika kutekeleza jukumu la kuimarisha ulinzi na usalama kupitia ulinzi shirikishi ambao umesaidia kupungua uhalifu ndani ya jamii.

ama
ALHAMISI AGOSTI 3, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



## Ndivyo uchafu unavyochafua sifa nzuri za Dar es Salaam

Ukurasa 14



## Mende mdudu mwenye karaha mkomeshe asiingie ndani kwako

Ukurasa 12

# Maabara zinaposhamiri kila kona wateja, wataalamu myasikie haya

Na Beatrice Philemon

Ni kawaida kukuta mabango yakitangaza huduma za maabara mitaani mijini na vijijini, tena wamiliki wakijinasibu kuwa wanafanyakazi hata kwa saa 24. Wateja huwakimbilia na kazi inaendelea.

Lakini, kuendesha maabara si jambo la kufanya kiholela bila usajili na uhakiki wa serikali. Ni huduma inayostahili kumulikwa na kuchunguzwa na adhabu za mtaalamu wa maabara anayefanya kazi bila usajili au kuandikishwa ni faini inayofikia hata Shilingi 1,000,000 na kifungo.

Mjumbe wa Sekretarieti ya Baraza la Wataalamu wa Maabara Michael Mtaki, anasema hayo na kufafanua kuwa faini ya awali ni Shilingi 500,000 hadi 1,000,000, kipo pia kifungo kati ya miezi sita hadi mwaka mmoja au mshitakiwa anaweza kupewa vyote kwa pamoja.

"Na kwa mwajiri anayeajiri ambaye hajasajiliwa anatozwa faini kati ya Shilingi 1,000,000 hadi i 3,000,000 au kifungo cha mwaka mmoja hadi mitatu au vyote viwili," anasema Mtaki.

Mtaki anasema hayo wakati anaelezea sheria inayosimamia taaluma ya Baraza la Wataalamu wa Maabara, kwenye mahafali ya sita ya wahitimu wa taaluma ya maabara katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala- Tanzania (KIUT) jijini Dar es Salaam.

Anawataka wahitimu kuzingatia maadili na miiko ya taaluma ikiwa ni pamoja na miongozo iliyowekwa ili kusaidia wananchi kupata majibu sahihi na huduma bora za afya wanapopimwa ili kujua matatizo yao na kupewa tiba sahihi.

Anahimiza kuacha kutoa vipimo vya uongo na kusisitiza kuwa



Mtaalamu wa maabara akiwa kazini . **PICHA: MTANDAO**

ni muhimu kuhakikisha majibu anayotoa yana ukweli, kuzingatia ubora kwenye vipimo atakavyochukua ili kumsaidia mgojwa kupata matibabu sahihi.

"Ninaomba wahitimu kujua sheria yetu inayosimamia taaluma ya Maabara kwani sheria hii ina jukumu la kuhakikisha mtaalamu anakuwa weledi kwa kusimamia kuanzia kule anakoandaliwa hadi kwenye utendaji wake wa kutoa huduma," anasema Mtaki.

Anataja makosa mengine kama kupotosha baraza kwa kutoa taarifa za uongo au nyaraka za kughushi ambapo akiwaeleza kuwa faini yake ni kati ya Shilingi 500,000 hadi 1,000,000 ama kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi 12 au vyote.

Aidha, anataja kufanya udanganyifu kwa kutumia jina au cheo kinachoashiria sifa ya kufanya kazi kama mtaalamu wa maabara za afya, kuitwa baraza na kushindwa kuhudhuria bila sababu za msingi ni mambo yanabeba adhabu.

Akitoa ujumbe kwa wahitimu watakaotaka kujiunga na baraza hilo kuwa taasisi hiyo inasajili kwa wataalamu wa shahada ya sayansi, stashahada ya juu au stashahada katika sayansi ya maabara za afya kutoka taasisi ya mafunzo inayotambulika na mamlaka za usajili na baraza na kuandikisha wahitimu ambao wamepata cheti katika sayansi ya maabara za afya kutoka taasisi ya mafunzo inayotambulika.

"Mtaalamu anapohitimu, anapaswa kuomba usajili wa awali ambao atautumia kufanya kazi chini ya usimamizi wa mtaalamu wa maabara na kuwasilisha vielelezo kwenye baraza ili aweze kuomba usajili wa kudumu au kuandikishwa akitaja kanuni ya 3 na 5-(3) kuwa ndizo zinazohusika.

"Baraza litampatia mtihani wa kumpima umahiri kabla ya kumpatia usajili wa kudumu au kuandikishwa," anaeleza Mtaki.

UKIKIUKA MAADILI

Wahitumu wa fani ya maabara wanakumbushwa kuwa endapo watakiuka maadili au kukutwa na hatia ya kosa la kitaalamu, wanaweza kuonywa au karipio, kusimamishwa kazi kwa muda au kufutiwa usajili, Mtaki akawaambia wakianza kufanya kazi wafuate sheria na miongozo.

Anawambia wahitimu na wanafunzi wengine wa mwaka wa kwanza, wa pili na watatu kuwa sababu zinazoweza kusababisha adhabu hizo ni pamoja na kushindwa kulipa ada ya mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, kuishi nje ya Tanzania Bara au kuondolewa kwenye rejesta kwa kosa lolote lile.

Mkuu wa Kitivo Mshiriki (Associate Dean) wa Chuo Kikuu cha KIUT, Profesa Ayoub Magimba,anawataka wahitimu kuwa mabalozi wazuri watakapokwenda kufanya kazi za maabara ka weledi.

"Mwende mkaonyeshe kwa vitendo vitu vyote mlivyosoma, fuateni miongozo iliyowekwa, kuna miongozo ya kitaifa na kimataifa kuweni na maadili mambo mengine yatafuata baadaye naamini mtakuwa wataalamu bora wa maabara," anasema Profesa Magimba.

Kwa upande wa vifaa vya maabara, chuo kitahakikisha mnapata vifaa vya kisasa vya maabara ili wanafunzi waweze kufanya majaribio na hatimaye kuzalisha au kutoa wanafunzi wenye ubora kwenye soko la ajira.

Anasema wahitimu hao watakwenda kufanya kazi katika maabara za tiba na kwamba kuna uhaba wa wafanyakazi kwenye idara ya tiba na kama mtaalamu au daktari hawezi kuwa na tiba shihi bila kujua ni aina gani ya vimelea au vidudu vinavyosaba-

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Mende mdudu mwenye karaha mkomeshe asiingie ndani kwako

**Na Mwandishi Wetu**

NYUMBA nyingi zimejaa mende ambao ni kero kutokana na kuchafua chakula, mazingira lakini pia ni waharibifu kwenye makabati ya vyombo na vyakula.

Lakini wataalamu wa wadudu wanasema kuwa ukifuata ushauri wao mende hawataingia kiurahisi nyumbani kwako.

Watu wengi hasa kinamama wanaogopa mende. Wewe ni mmoja wao? Ukiona anaruka unaogopa na hata kukimbia ovyo?

Katika makala hii ya BBC, mwoga wa mende anasema alipokuwa na umri wa miaka sita, alikuwa akitoa kitu jikoni, mende aliporuka na kutua kwenye shingo yake alipiga kelele kwa woga na kudondosha chupa ambayo ilivunjika. Na pia aliwaona mende.

"Nyumbani kwetu, kaka na dada zangu hucheza na mende. Ukweli nachukizwa.

Kwa kweli, inavyoonekana sasa ni kwamba watu hawahitaji kuogopa mende." Anasema.

Ni kwa sababu hawanyonyi damu za binadamu kama walivyo mbu na wadudu wengine wanaodunga kama kunguni au kupe.

Hata hivyo, anasema Bronoy, mtaalamu wa wadudu katika Taasisi ya Utafiti wa Ikolojia ya Misitu, mende hao huishi katika maeneo yenye uchafu.

"Kwa kawaida mende hupatikana sehemu chafu, majalalani, vyooni na mabaki ya vyakula yanayotupwa ovyo, ndiyo maana wanachukiwa na watu wengi," anasema Bronoy.

Anafafanua kuwa hofu ya magonjwa kutoka kwenye mende ilianzia Ugiriki ya zama za kale.

"Wakati wa Wagiriki wa kale, mende walihofiwa kusababisha magonjwa ila wadudu hao wana protini inayoitwa tropomyosin.

Wataalamu wanasema protini hiyo kwenye kinyesi cha mende, ngozi na sehemu za mwili wake inaweza kusababisha mzio au aleji kwa binadamu, kwa mujibu wa Bronoy.

Halikadhalika Wamisri wa kale waliabudu miungu ili kuwafukuza mende na katika maneno ya kimatibabu 'hofu' au 'kuchukia' mende hujulikana kama 'Catasaridaphobia'.



**KUENEZA MARADHI**

Lipo swali kuwa magonjwa huenezwaje na mende? Jibu analo Selva Muthu Kumaran, Profesa Mshiriki wa Idara ya Entomolojia ambayo ni elimu na utafiti wa kisayansi kuhusu wadudu, anasema kwamba mende hawaambukizi ugonjwa wowote moja kwa moja kwa wanadamu.

Malaria na dengue huenezwa na mbu wakati kipindupindu inzi anahusika lakini tauni huenezwa na panya.

Anaongeza kuwa mende hawasambazi magonjwa moja kwa moja kwa wanadamu, ila vitu vinavyooza ambavyo mende hula vina vijidudu.

Baada ya kula hivi vitu, mende wanapoingia kwenye chakula wanachokula, vimemea na wadudu hao huchanganyika na vyakula na kuwasababishia magonjwa wanadamu," anasema Selva.

**UTAWADHIBITIJE**

La muhimu ni kujua namna ya kudhibiti mende kuingia kwenye nyumba na hapo

Selva anaeleza kuwa mende huishi vyema na kufurahia mahali penye chakula na mazingira yenye unyevunyevu, na kwamba usafi ukifanyika kikamilifu hawatakuja.

Anawahimiza watu kuosha sahani na vyombo vilivyotumiwa kula na kuandaa chakula mara moja.

Aidha, anakumbusha kuwa chakula chochote kilichobaki kinapaswa kutupwa au kuhifadhi mara moja siyo kuachwa juu ya jiko, mezani au kwenye sufuria na vyombo vya kulia au kuandaa.

Anasema kuhakikisha kwamba takataka hazikusanyiki ndani ya nyumba ni jambo jema kudhibiti mende.

Kadhalika mapipa au ndoo za takataka unazotumia yanapaswa kufungwa au kufunikwa kikamilifu.

Lakini pia yawekwa nje ya nyumba usiku na kuhifadhiwa kwenye maeneo safi.

Anakumbusha kuwa mende wanaweza kuingia kupitia madirishani na milangoni, kwa hivyo unapaswa kufunga milango na madirisha wakati hauyatumii.

Makabati na masanduku ya mbao ni kivutio kwa mende, uangalifu ni muhimu kwa sababu kuna aina ya mbao kwao ni chakula bora kwa mende ndiyo maana wanaishi kwenye kabati.

Selva anasema mende wengi huingia majumbani kupitia macaroni ,kwa hivyo, ni bora kuyatunza na kuyafunika wakati wa usiku na kuzuia kila upenyo wanaoweza kuutumia.

Dawa za kupuliza hutumiwa kufukuza mende kutoka ndani ya nyumba. Hata hivyo, matumizi zaidi ya dawa za aina hizi yanaweza pia kuwa na madhara kwa wanadamu na ikolojia, hivyo usafi ni muhimu kuliko kemikali za sumu.

**BBC**

## MAABARA ZINAPOSHAMIRI KILA KONA WATEJA, WATAALAMU MYASIKIE HAYA

Inatoka Uk. 11

bisha ugonjwa na kuwataka kuwa makini na weledi.

Profesa Magimba anaahidi kuwa chuo kitaendelea kuzalisha wataalamu wabobezi wa fani ya maabara na katika sekta ya afya kukabiliana na uhaba wa wafanyakazi kwenye idara ya tiba, na kwamba huwezi kuwa na tiba bora bila kujua ni vijidudu au vimelea gani vinaathiri afya ya mgonjwa au kugundua ni aina gani ya vimelea au vijidudu vinavyosababisha maradhi akiwamo wahitimu kutumia ujuzi walioupata chuoni kutoa majibu sahihi wanapochukua vipimo kwa mgonjwa.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Kitaalamu Afrika Mashariki (MELSAT), Yahya Mnunga, akizungumza katika mahafali hayo anasema watalaamu wa maabara ndiyo nyenzo kubwa kwa taifa ili wananchi wake wawe na afya njema na uchumi kukua.

"Wataalamu hawa wataongeza nguvu katika sekta ya afya, wafanye kazi kwa weledi na changamoto zilizopo serikali itazifanyia kazi," anasema Mnungu.

Hadi sasa watalaamu wa maabara nchini wapo 15,000, kati ya hao, 6000 wapo kwenye ajira rasmi na waliobaki wapo mitaani pengine kwenye hospitali binafsi au bado hawajapata ajira, anasema.

"Kwa sababu idadi kubwa ya watalaamu wa maabara wanaomaliza masomo inazidi kuongezeka. Naomba serikali kama ikifika muda wa kuajiri wawafikirie hawa watalaamu kwa sababu imejenga vituo vingi vya afya katika mikoa na wilaya ili wakatoe huduma za kimaabara na kusaidia kuboresha afya za Watanzania."

Mbali na hilo anawahimiza wahitimu kujiunga na MELSAT sehemu itakayowasikiliza , kutatua changamoto za kitaaluma na kujali maslahi ya wanataaluma hao.

"Magonjwa hayana mipaka, mjenge umoja na ushirikiano, mjitambue na mjue wapi mnakwenda, wahitimu ni wengi kuliko maeneo tunayokwenda kufanyia kazi, unaweza kuajiriwa serikalini, sekta binafsi au ukaamua kujikita kwenye eneo la utafiti na ukaandika andiko lako zuri la kuanzisha mradi ukaleta MELSAT na sisi tutakusaidia kupata mtaji wa kuanzisha mradi badala ya kuendelea kutegemea ajira." anasema.

"MELSAT itawasaidia kupata mikopo bila dhamana, hii ni fursa kubwa mnaweza kuitumia kwa kujiunga kwenye kikundi na hatimaye mkaweza hata kuanzisha 'Diagnostic Centre" kituo cha kuchuynguza magonjwa au mkaangalia fursa nyingine katika eneo hili." Anawaambia wahitimu.

Mnungu anawataka madaktari kufanya kazi kwa ukaribu na wataalamu wa maabara kwa sababu ndiyo wanaopima kugundua vimelea gani au vijidudu gani na hatimaye kuwawezesha madaktari kutoa tiba sahihi.

AFYA

# Ni Bukoba bila athari za Marburg hakikisho la Msalaba Mwekundu

## •Watumia wafanyakazi 202 kufunza watu



Mratibu wa mambo ya huduma ya kwanza wa Chama cha Msalaba Mwekundu, Kheri Issa, akizungumzia utoaji wa elimu kudhibiti ugonjwa wa Marburg Bukoba. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

MARBURG ni maradhi yaliyoibuka mkoani Kagera, Machi mwaka huu na kusababisha vifo vya wagonjwa sita kabla ya serikali na wadau mbalimbali kuukabili na kuudhibiti.

Haya ni maradhi ya virusi vya Marburg, ambavyo ni hatari sana unaosababisha homa na kutokwa damu kila sehemu yenye uwazi mwilini. Wataalamu wanaeleza kuwa uwiano wa vifo vya walioambukizwa inafikia hadi asilimia 88 ikimaanisha kuwa watu 100 wakiugua karibu 90 wanakufa.

Marburg ni virusi vya jamii au familia moja na virusi vinavyosababisha Ebola, kwa mujibuwa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Wakati Marburg iliporipotiwa mkoani Kagera WHO ilitangaza uwapo wa maradh haya nchini Equatorial Guinea Machi 23, mwaka huu.

Katika kukabiliana na maradhi hayo na kuongeza uelewa wa udhibiti, Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, 'Red Cross', kilendelea na kambi kuuelimisha umma kuhusu ndwele hizo ambazo zilipolipuka hazikujulikana.

Baada ugonjwa huo kudhibitiwa, Msalaba Mwekundu uliamua kubaki mkoani humo kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kaya kwa kaya ili wajue athari za ugonjwa huo na jinsi ya kujikinga nao na kuhitimisha kazi hiyo ya miezi mitatu Julai 31 mwaka huu.

Mratibu wa mambo ya huduma ya kwanza wa chama hicho, Kheri Issa, anaeleza hayo, wakati akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, mara baada ya kurejea kutoa mkoani Kagera kufuatilia maendeleo ya elimu inayotolewa na wafanyakazi wao.

"Red Cross tulitoa mafunzo kwa wafanyakazi 202 wa kujitolea ambao walibaki mkoani Kagera wakiwapa elimu kaya baada ya kaya yenye lengo la kujengea wananchi uelewa, ili hata kama ugonjwa huo utarudi, wawe na uwezo wa kukabiliana nao kabla haujaleta madhara zaidi," anasema.

Anafafanua kuwa ugonjwa huo kumalizika haina maana kuwa hautaweza kurudi tena, na kwamba waliwaacha wafanyakazi wakiendelea kutoa elimu ili jamii itambue na kuachana na tabia zinazoweza kusababisha urejee.

"Kwa hiyo wameelimisha jamii kuzingagtia suala la usafi wa mazingira, wa maji, kunawa mikono kwa kutumia sabuni na vitakasa mikono, lakini pia walikuwa wakipewa nafasi ya kuuliza maswali na kujibiwa ili waweze kuelewa zaidi," anasema.

> **"Red Cross tulitoa mafunzo kwa wafanyakazi 202 wa kujitolea ambao walibaki mkoani Kagera wakiwapa elimu kaya baada ya kaya yenye lengo la kujengea wananchi...**

Mratibu huyo anafafanua kuwa wakati ugonjwa unapamba moto, kulikuwa na wadau mbalimbali walioshirikiana na serikali, lakini baada ya kudhibitiwa, wakabaki wao na watumishi wa serikali wakiendelea kutoa elimu.

Issa anafafanua kuwa wadau wa afya waligawanyika katika vikosi kazi zaidi ya sita vya kazi kwa mfano cha matibabu, ili kuepuka maambukizi, maabara na uchunguzi, cha ufuatiliaji wa waliohisiwa kuwa na ugonjwa au waliohifadhiwa sehemu moja kama wana dalili.

"Kikosi cha nne kilikuwa ni cha kuelimisha umma, kuonyesha wananchi ubaya na athari, elimu ilitolewa kwa njia ya vipaza sauti katika mikusanyiko, kwenye myalo au kambi za wavuvi, nyumba za ibada na kila eneo wanajamii, lakini wafanyakazi wa kujitolea waliokuwa wakiendelea na elimu hiyo wakiingia kaya kwa kaya," anasema.

Mratibu huyo anakitaja kikosi cha tano kwamba kilikuhusika na suala la maji, usafi wa mazingira, ili kukabili ugonjwa, ukaguzi wa wasafiri kutoka mkoani Kagera kupima joto la mwili la kila msafiri ili kubaini kama kuna tatizo ili ashughulikiwe.

"Kikosi kazi kingine kilikuwa ni cha saikolojia kwani watu walihitaji msaada huo wakiwamo waliowekwa sehemu maalum au kaya zilizopoteza wapendwa wao. Msaada huo pia ulikuwa ukiwanufaisha watumishi kuwaweka sawa, kwani kuhudumia mgtu mwenye ugonjwa huo wanaweza kuathirika kisaikolojia," anasema.

Anazungumzia kingine kilichohusika na kutunza zana zote za kufanyia kazi kama vipima joto, magari, mavazi maalum ya kujinga na ugonjwa na kwamba ziliwekwa sehemu moja na kila zilipohitajika zilichukuliwa na kwenda kutumiwa.

Mwanzoni mwa Juni mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anatangaza rasmi kuisha ugonjwa wa marburg ambao ulisababisha vifo vya wananchi sita kutoka katika kata za Maruku na Kanyangereko mkoani Kagera.

Waziri anasema Tanzania ipo salama kwa umoja, nguvu na ushirikiano wa pamoja wameweza kuuthibiti ugonjwa huo ambao awali ulipoingia mkoani humo, ulikuwa haujajulikana.

Anaongeza kuwa jitihada za pamoja za serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa sekta ya afya na wa kimataifa wameweza kutokomeza ugonjwa ndani ya kipindi kifupi.

Ummy anasema ni fahari Watanzania kwamba wameweza kulinda na kutimiza wajibu wao wa kimataifa wa kuilinda dunia dhidi ya ugonjwa huo huku akishukuru Shirika la Afya Duniani hapa nchini kwa kuongoza wadau wa kimataifa katika mapambano hayo.

Hata hivyo, anatoa wito kwa wananchi kuwa macho wakati wote, ili kama kutakuwa na tetesi za mhisiwa au mtu mwenye dalili za ugonjwa wowote usio wa kawaida ama unaotia mashaka, watoe taarifa haraka.

MAZINGIRA

# Ndivyo uchafu unavyochafua sifa nzuri za Dar es Salaam



Ndivyo mto unavyopambwa na taka: **PICHA MTANDAO**

**Na Anthony Gervas**

DAR-ES SALAAM moja ya majiji makubwa na mlango wa kibiashara Afrika Mashariki inasifiwa kwa mengi. Mosi, ina wakazi wakarimu, ipo jirani na bahari na muhimu ni makazi yenye amani wakati wote. Lakini, sifa zote zinatibuliwa na uchafu.

Ni jiji lenye wakazi zaidi ya milioni 5,000,000 na changamoto ya uchafuzi wa mazingira katika maeneo mengi kuanzia katikati hadi kwenye mitaa, barabara na mitaro ya maji taka ni ugonjwa usiopona.

Mathalani, kuna mkondo wa maji uliopo Yombo Kilakala Manispaa ya Temeke, huu umechafuka kiasi cha kubadilisha mazingira ya asili wakiwamo viumbe na mimea ambavyo huenda vimetoweshwa.

Uchafuzi huo unasababishwa na kutupa taka ovyo kutoka katika makazi ya watu na maeneo mbalimbali jirani na mikondo ya maji, mitaro na mifereji mikubwa inayosafirisha maji kutoka eneo moja kwenda jingine hatimaye kuingia katika Bahari ya Hindi.

Jicho la Nipashe limetua katika mkondo wa maji unaopita Yombo Kilakala na kuunganisha daraja la Tingetinge Relini, huko Temeke, chanzo chake kikiwa ni Vingunguti huko Kiwalani kupitia Sandali na maeneo ya Mtaa wa Nyambwela hadi Tandika.

Mkondo huo unadaiwa kumwaga maji yake Mto Mzinda kupitia Yombo hadi Kurasini ambayo husafirishwa hadi kuingia baharini. Umejaa tope zito na taka za aina zote ambazo zinatisha machoni unapoangalia.

Wakazi wanaishi kando kando maeneo hayo na hata wengine wengi wameugeuza mkondo kuwa dampo bila kujali usafi wa mazingira na afya zao.

Uchafuzi huo,unaosababisha kuwepo harufu mbaya wakati wote mwaka hadi mwaka na ni mateso kwa anayepita kwenye daraja hilo na wakazi wa pembezoni .

### WANAKWAMA WAPI?

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Kilakala Ally Jabir, anasema ofisi yao inatoa elimu kwa wananchi kila mara juu ya utunzaji mazingira kwa kuweka taka kwenye viroba baadaye Kampuni ya Mkombozi Investment, iliyopewa jukumu la kukusanya taka mitaani hupita na kuzoa taka hizo.

"Wananchi wanatakiwa kutunza mazingira kwa kufanya usafi kila eneo au mitaa yao,taka ziwekwe kwenye viroba ili watoa huduma ya kuzoa, waliopewa kazi hiyo wazipitie na kukusanya kupeleka dampo,"anasema Jabir.

Anasema wapo wananchi wakorofi ambao hutupa uchafu bila kujali afya za wengine ikiwemo kutupa chupa za plastiki za maji, taka nyingine ngumu kuanzia matairi, magodoro, viambato vya simu kama betri zake, makasha na hata vifaa vya kielektroniki.

Taka hizo husambaa ndani ya mkondo wa maji na maeneo ya jirani kwenye makazi na akaeleza kuwa wanaotupa huvizia nyakati za usiku ili kubeba viroba na ndoo chakavu za plastiki hata wenye magari wanaweza kufikisha viroba na mafurushi ya uchafu.

Jabir anasema kadhalika ofisi ya serikali ya mtaa imeshatoa jukumu kwa wajumbe wa mashina kuhakikisha wanasimamia na kukabili uchafuzi wa mazingira hususan katika maeneo hayo.

Anaongeza kuwa pia walishakabidhi jukumu la usimamizi na usafi wa mazingira katika kamati ya afya na mazingira ya mtaa wa Kilakala.

### KUTUNGA SHERIA

Jabir anasema serikali ya mtaa huo ilishatunga na kuwasilisha mapendekezo ya sheria ndogo ndogo za kuwaadhibu wakorofi wanaokaidi na kufanya uchafu kila wakati,ambayo yanasubiri kupitishwa kwenye mkutano wa mtaa mwezi ujao wa Septemba,

Anasema wanachukua hatua hiyo ili kubaki na jukumu kuu la kusimamia masuala ya ulinzi na usalama,maendeleo ya wananchi,miundombinu na utatuzi wa migogoro katika jamii ya Kilakala.

Anaendelea kusisitiza suala la utoaji elimu kwa wananchi, akikazia kwamba,muhimu sana kuendelea kutolewa,kisheria kuchukuliwa wanaokaidi kutekeleza jambo hilo.

Anataja changamoto zinazowakabili pia wananchi mtaani,ukiwemo ukosefu wa makaro yakuhifadhia maji machafu,ambayo hutitirika kutoka kwenye majumbani hadi kuingia kwenye mikondo ya maji,mitaro au mito,kukosa vizimba vya kuhifadhia taka hizo kwa ajili ya kusubiri kuzolewa.

### WANA MAZINGIRA.

Katibu wa Kamati ya Afya na Mazingira Mtaa wa Kilakala, Seif Mchila, anafafanua kuwa mkondo huo husafirisha maji hadi Bahari ya Hindi.

"Sisi hatua tunazochukua ni kuzungukia maeneo yote ya mkondo ule, na kutoa elimu kwa wananchi,mfano,mwezi Juni tulifanya zoezi kamati yetu kuhakikisha tunafanya usafi wa kuondoa taka na uchafu wote likiwamo tope linalojaa ndani ya maji na kubadilika rangi.

Aidha, tumeweka sharti mtu akikamatwa anatupa taka ovyo anaonywa na kuzoa taka hizo alizokuja nazo ,anasema Mchila.

Kadhalika anazungumzia changamoto kubwa akisema bado huchangiwa na wananchi,wanasiasa,na viongozi wengine wa mitaa,wakiwemo wajumbe wa mashina wanaoshindwa kukemea uchafuzi ule na kusimamia maeneo yao.huku akisema kauli mbiu yao ni "afya yangu mtaji wangu,anasema..

Shaban Ally ni Ofisa Mtendaji Mtaa wa Kilakala anayeleza kuwa ofisi yake walishagawana majukumu na Kamati ya Afya na Mazingira,wao wamebaki na kusimamia serikali ya mtaa lakini wako nao pamoja katika kushiriki shughuli zingine za maendeleo, huku akijidai kuwa hivi sasa wameshapata Mashine ya Kielektroniki (EFD),kwa ajili ya kuwatoza faini wanaokamatwa wakitupa uchafuzi huo.

Faini ya wakosaji itakuwa Shilingi 50,000 ikiwa sehemu ya adhabu kali ili kukomesha tabia za watu wasiojali usafi wa mazingira na afya za wananchi,asipokoma mhusika anafikishwa katika mahakama ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke au kwa mawakili wa Mahakama ya Jiji.

Wananchi katika hoja ya usafi wa mazingira wanakiri kuunga mkono,sababu ni changamoto ambayo ni pasua kichwa mtaani kila siku kero ya uchafuzi huo,huku wakiomba serikali kusaidia kutoa msaada wa vifaa vya kufanyia usafi katika mkondo huo wa maji na maeneo ya makazi ya watu ili kujikinga na hatari ya afya zao.

Mkazi wa eneo la Kilakala Msibishe Mjumba,anadai kwamba uchafuzi wa mazingira unasababishwa na utamaduni wa watu walizoea kuishi hivyo tangu zamani,sasa kuwabadilisha umekuwa mtihani kwa serikali.

"Watu tangu zamani walizoea utamaduni wa kuchafua,kutupa taka ovyo ilikuwa jadi yao bila kujali madhara yake, hiyo ndiyo shida kubwa inayoendela kusumbua,kikubwa ni kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na viongozi,kukagua maeneo mikondo ya maji,mifereji na mito jambo muhimu siyo kutangaza kwenye spika tu haiwezi kusaidia,anasema Msibishe.



# Singida yatangazwa kinara utekelezaji miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MANISPAA ya Singida imetangazwa kuwa kinara katika utekelezaji wa miradi ya BOOST kwa kujenga majengo yake kwa viwango bora.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumza juzi wakati wa hafla ya makabidhiano ya miundombinu ya elimu iliyojengwa kupitia mradi wa BOOST mwaka 2022/2023, alisema mkoa huo ulipata Sh. bilioni 9.2 kwa ajili ya miradi hiyo.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imeshika nafasi ya pili ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambayo imeshika nafasi ya tatu, Manyoni nafasi ya nne na Itigi nafasi ya tano huku nafasi mbili za mwisho zimeshikwa na Halmashauri ya Iramba na Ikungi ambazo zilishindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Serukamba alisema katika utekelezaji miradi hiyo ya BOOST zimejengwa shule mpya 12 za msingi, madarasa 305, matundu ya vyoo 420, nyumba za walimu wawili na majengo ya utawala 12.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskasi Muragili, alisema wanafunzi 2,745 wa shule za msingi katika Manispaa ya Singida, watanufaika kutokana na uwapo wa vyumba vya madarasa 61 vipya, matundu ya vyoo 49, vyumba vya madarasa ya awali sita na majengo mawili ya utawala.

Alisema kuwapo kwa miundombinu hiyo ya kujifunzia siyo tu itapunguza kwa kiasi kikubwa msongamano wa wanafunzi madarasani, lakini kuwawezesha wanafunzi hao kufuatilia masomo kwa utulivu kutokana na uwapo wa madawati kulingana na idadi ya wanafunzi katika vyumba vya madarasa hayo mapya.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, aliwapongeza walimu na watendaji ambao walivaa viatu vya wahandisi kwa kusimamia vyema mradi wa BOOST na kuwaasa kuwa kazi iliyobaki ni kuleta matokeo mazuri ya ufaulu kwa wanafunzi.

# FCC yabaini makasha bandarini kukutwa bidhaa zilizokiuka sheria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Ushindani (FCC) imefanya ukaguzi katika bandari ya Dar es Saalam na bandari kavu na kubaini asilimia 3.4 ya makasha yenye thamani ya Sh. bilioni 20.8 yalikaguliwa na yalikutwa na na bidhaa zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa.

Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Erio, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume hiyo na mwelekeo wa utekelezaji wa mwaka wa fedha 2023/2024.

Erio, alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 mapambano dhidi ya bidhaa bandia nchini yalikuwa ni pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali katika bandari ya Dar es Saalam pamoja na bandari kavu.

Aidha, alisema ukaguzi wa kushtukiza uliofanyika bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 4.7 zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa zilikamatwa na hatua stahiki kuchukuliwa.

"Kaguzi hizo zilifanyika katika mikoa ya Dar es Saalam, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Songwe, Kilimanjaro, Pwani, Mwanza, Arusha, Katavi na Mbeya," alisema Mkurugenzi huyo.

Kadhalika, alisema FCC, imefanya uharibifu wa bidhaa zilizokamatwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa na Ruvuma bidhaa zilizoharibiwa ni pamoja na wino wa printa katoni 432 na kilo 1,302 za vifungashio.

"Kaguzi hizi zinapunguza madhara ya bidhaa bandia ambazo pamoja na mambo mengine zinaweza kutokuwa salama kwa walaji, zinaikosesha serikali mapato na zinaweza kuathiri biashara na uwekezaji halali nchini," alisisitiza.

Alisema walaji wanatakiwa kufahamu kuwa watengenezaji wa bidhaa bandia huwa wanatengeneza kwenye majina yanayouzika kwa uhalisia zenye kukubalika sokoni.

"Hivyo ni vizuri walaji wajifunze mbinu za kuzitambua bidhaa bandia kwa kufanya milinganisho ya bei pamoja na kufuata maelekezo ya alama za bidhaa zinazotolewa na kampuni husika inayomiliki nembo ya bidhaa halali," alisisitiza.

Vile vile, alisema FCC kwa kushirikiana na mamlaka zingine zinazohusika imeendelea kutoa elimu kwa walaji na wasambazaji wa bidhaa hizo bandia wanaelekezwa kujirekebisha na kutengeneza zenye nembo zao binafsi sokoni.

Akizungumzia mafaniko katika sekta ya biashara Erio, alisema FCC ilitoa onyo kwa wazalishaji wa sukari kutokana na kubainika kuwepo kwa viashiria vya upangaji bei na kupunguza usambazaji hasa katika vipindi vya mwezi mtukufu wa Ramadhani.

"Onyo hilo lilisababisha bei ya sukari sokoni kuimarika na upatikanaji wa bidhaa husika kuongezeka," alisema.

Kuhusu kuboresha mazingira ya uwekezaji alisema FCC, iliongeza kizingiti cha kuruhusu miungano ya Kampuni kutoka Sh. milioni 800 kwenda Sh. bilioni 3.5 hatua iliyowezesha wawekezaji wadogo na wa kati kuunganisha shughuli zao za kibiashara bila kuhitaji idhini ya FCC.

Hata hivyo, alisema hatua hiyo imewezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kukuza mitaji yao na teknolojia.



Mkurungenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC), William Erio (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya tume hiyo katika mwaka wa fedha 2023/2024. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana 1,000 kushiriki kongomano uongozi/utawala bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIJANA 1,000 nchini leo wanatarajia kushiriki kongamano la maendeleo ya vijana linalolenga kujadili masuala ya uongozi na utawala bora ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Akizungumza jana jijini hapa na waandishi wa habari, Ofisa Maendeleo ya Vijana Mwandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Amina Sanga, alisema litafanyika kwa siku mbili na vijana watapata fursa za kufahamu masuala yao na ni utekelezaji wa sera ya vijana.

"Sera ya vijana inatutaka tuwakutanishe vijana kwa ajili ya makongamano ya kuzungumzia fursa na masuala yanayotekelezwa na serikali, watajifunza kutoka kwa vijana wengine wa ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema serikali inaunga mkono makongamano hayo na kuwahamasisha vijana kushiriki kwa wingi kwa kuwa ni fursa muhimu kwao.

Awali, Mkurugenzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Vijana Dodoma (DOYODO), Rajab Nonga, alisema kongamano hilo pia litashirikisha vijana kutoka nchi za Afrika Mashariki.

"Katika kongamano hili kuna uwakilishi wa vijana kutoka makundi mbalimbali kama vile bodaboda, wajasiriamali, watu wenye ulemavu na hakuna kijana yeyote atakayeachwa nyuma kwenye kongamano hili," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amesisitiza kuwapo na majukwaa ya kuwakutanisha vijana ili kujadili sera, sheria na kutoa maoni yao.

"Tumekuja na mkakati huu wa kuwaleta vijana pamoja na kongamano limeshirikisha mashirika 32 na wizara za kisekta," alisema.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Freedom House, Daniel Lema, alisema vijana watatoka na maazimio yatakayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

"Tutajadili masuala ya vijana na uchumi, vijana na uongozi, vijana na utawala bora, fursa za kiuchumi kwa vijana, suala la afya ya akili kwa vijana litajadiliwa ambalo limekuwa ni changamoto inayowakabili vijana kwasasa."

"Tutajadili kuhusu vijana na upatikanaji wa rasilimali fedha kupitia fursa zilizopo kama mfuko wa maendeleo ya vijana, mikopo ya halmashauri na asilimia ile inayotengwa kwenye ununuzi wa umma," alisema.



# Halmashauri yapoteza mil. 500/- kodi vibanda

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya, imepoteza zaidi ya Sh. milioni 500 za mapato yatokanayo na kodi ya vyumba vya biashara na ushuru katika kipindi cha miaka saba kutokana na soko la Tunduma Road lililoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kutofunguliwa licha ya kukamilika.

Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Daudi Mbembela, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa agizo la Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kuhusu kufunguliwa kwa soko hilo.

Julai 26, mwaka huu, Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Mbeya, iliuagiza uongozi wa halmashauri hiyo kulifungua soko hilo na kuwaondoa wajasiriamali wanaofanya biashara kwenye masoko yasiyo rasmi na wanaofanyia shughuli zao kwenye maeneo ya hifadhi za barabara.

Juzi, soko hilo lilifunguliwa na baadhi ya masoko yasiyo rasmi yalianza kufungwa huku ikifanyika oparesheni ya kuwaondoa wajasiriamali barabarani na kuyahamishia baadhi ya magari kwenye eneo hilo. Mbembela alisema soko hilo lina vizimba 521 ambavyo kila kimoja kinatakiwa kulipiwa Sh. 2,000 kwa mwezi na ushuru wa Sh. 500 kwa siku, hivyo kwa mwezi wanapoteza zaidi ya Sh. milioni 94 kama kodi na ushuru.

Pia alisema soko hilo lina vyumba 195 vya biashara ambavyo kila kimoja kinatakiwa kulipiwa sh. 25,000 hivyo katika kipindi cha miaka saba wamepoteza zaidi ya Sh. milioni 400.

Alisema kwa sasa baada ya kulifungua soko hilo, wameamua kuwapa wananchi mwezi mmoja wa kufanya biashara bila kulipia chochote kwa lengo la kutoa elimu na kuweka mazingira rafiki zaidi.

"Tunashukuru tayari tumeshalifungua soko letu na kama mlivyoona wajasiriamali wanaendelea na biashara zao humo ndani, hapa tumeshagawa vizimba na vibanda na tutasimamia ili kuhakikisha soko letu linakwenda vizuri," alisema Mbembela.

Alisema wameshaanza kuchukua hatua kwa wale wanaokaidi kuondoka kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi kwa kuwapeleka polisi na kuwafungulia kesi akidai kuwa serikali haipati chochote kwenye maeneo hayo.

Mwenyekiti wa CCM Kata ya Tunduma Road, Michael Ngalya, alisema barabara inayounganisha soko hilo na barabara kuu imeshachongwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kama sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Siasa ya chama hicho. Alisema kwa muda mrefu serikali imekuwa ikitoa maagizo ya soko hilo kufunguliwa lakini hakukuwa na utekelezaji wa aina yoyote kutokana na sababu ambazo zilikuwa hazieleweki.

Miundombinu ya soko hilo, alisema ilishakamilika muda mrefu lakini kufunguliwa kwa soko ilikuwa mtihani kwa viongozi wa eneo hilo kutokana na mivutano iliyokuwapo.

"Tunashukuru Kamati ya Siasa ilipokuja hapa ilitoa maagizo kwa TARURA kukwangua barabara hii na ilipofika Ijumaa kweli walianza kufanya kazi na kama mnavyoona kazi inaendelea hapa," alisema Ngalya.

Baadhi ya wajasiriamali wanaofanya shughuli zao kwenye eneo hilo walisema soko hilo ni eneo sahihi kwao kufanyia shughuli zao kutokana na maeneo ya barabarani walimokuwa wanafanyia kazi kuwa hatarishi. Mmoja wa wajasiriamali hao, Rebeca Mwamahonje aliomba Serikali kuweka msimamo mkali kwa kuhakikisha wajasiriamali walioingia kwenye soko hilo hawaondoki tena kama ilivyowahi kutokea awali.



Ofisa Biashara Mkuu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) Nyanda za Juu Kusini, Noah Kitulo (kulia), akizungumza na mzee Amon Mwangosi (aliye juu ya trekta) anayejishughulisha na kilimo cha mahindi, maharagwe, alizeti na soya, alipotembelea banda la benki hiyo, katika maonyesho ya Nane Nane 2023 kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TADB yajinadi kuwakomboa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

IKIWA ni sehemu ya kuwafikishia wakulima fursa mbalimbali ikiwamo mikopo ya riba nafuu, mafunzo na ushauri wa kitaalamu, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inashiriki maonesho ya wakulima 'NaneNane' yanayoendelea jijini hapa katika Viwanja vya John Mwakangale.

Maadhimisho ya Nanenane, ambayo huenda sambamba na maonesho ya kilimo, hufanyika kila mwaka ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wa wakulima kwa uchumi wa nchi. Maonyesho hutoa pia fursa kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo kuonesha shughuli zao za kilimo kwa umma.

Meneja Mawasiliano na Masoko wa TADB, Amani Nkurlu, aliliambia gazeti hili jana jijini hapa kuwa benki hiyo inashiriki maonyesho hayo makubwa ya kilimo kwa mara nyingine na kuwataka wakulima na wadau mbalimbali kufika katika banda lao kujifunza namna inavyosaidia sekta ya kilimo nchini.

"Huu ni mwendelezo wa TADB kushiriki maonyesho ya Nanenane kila mwaka. Kwetu sisi, maonyesho haya ni muhimu sana kwa kuwa hutuwezesha kukutana moja kwa moja na wakulima na wadau mbalimbali kutoka kila kona ya nchi," alisema.

"Kupitia TADB, wakulima wanaweza kupata mikopo ya muda mfupi, muda wa kati na mrefu kwa riba nafuu zaidi katika soko hadi kufikia asilimia tisa. Tunatoa huduma zetu kwa wakulima na wafanyabiashara katika sekta ya kilimo kwenye mnyororo mzima wa thamani ikiwemo sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi," aliongeza Nkurlu.

Alisema benki hiyo pia inatoa mikopo kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS) kwa kushirikiana na mabenki washirika ya kibiashara ili kuhakikisha wakulima wadogo wengi zaidi wananufaika na mikopo ya riba nafuu, ambapo TADB inachukua jukumu la kutoa dhamana kwa wakulima hao.

# Watanzania wakumbushwa kuwaenzi waasisi wa taifa

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WATANZANIA wamepewa wito wa kuwaenzi waasisi wa taifa waliokuwa mstari wa mbele kwenye harakati za ukombozi wa Tanganyika kwa kuwa wazalendo na wenye kufuata maadili.

Mmoja wa wazee mkoani Mbeya. Stephen Mwakangale, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Banda la Kumbukumbu ya John Mwakangale, katika Maonyesho ya Kitaifa ya Nanenane mwaka 2023 yanayofanyika jijini hapa, ndani ya viwanja vya John Mwakangale.

Stephen ambaye ni mtoto wa kwanza wa John Mwakangale, alisema baba yake ni miongoni mwa wanasiasa waasisi wa iliyokuwa Tanganyika African National Union (TANU), aliyeungana na Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania, katika kulipambania taifa.

"John Mwakangale na Mwalimu Nyerere walikuwa karibu sana. Kuna wakati Mwalimu alipokuwa akisoma Scotland alikutana na baba yangu ambaye naye alikuwa masomoni Uingereza. Walikutana huko na kukubaliana kuja kuendeleza harakati za TANU," alisema.

"Wakati tunapata Uhuru mwaka 1961 baba (John Mwakangale) alikuwa mbunge. Hata hivyo, Desemba 1962, Mwalimu Nyerere alimteua Mwakangale kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati huo Mbeya ikiitwa Mkoa wa Southern Highlands, ikijumuisha mikoa ya sasa Songwe, Njombe, Iringa, Rukwa na Katavi," aliongeza.

Alisema lengo la kuonyesha kumbukumbu za John Mwakangale, kwenye maonyesho hayo ni kuonyesha historia ya Mwakangale tangu harakati za ukombozi wa Tanganyika chini ya TANU, Uhuru hadi Chama Cha Mapinduzi (CCM). "Lengo la kuonyesha kumbukumbu za John Mwakangale ni kuhamasisha na kuirithisha jamii mazuri ambayo yalifanywa na waasisi wa taifa letu kwa kutambua mchango wao kabla na baada ya uhuru. Mchango wao kwenye kilimo, siasa na uchumi unapaswa kukumbukwa kizazi hiki na kijacho.

"Ametambuliwa na viongozi tofauti maarafu. Nelson Mandela, kwenye kitabu chake kiitwacho 'LONG WALK to FREEDOM' amemwelezea John Mwakangale na namna alivyompokea mkoani Mbeya mwaka 1962 kabla ya Mandela kwenda Addis Ababa, Ethiopia kushiriki mkutano wa Muungano wa Ukombozi Kusini na Mashariki mwa Afrika (PAFMECA)," alisema Stephen.

Alisema kwamba kabla ya uhuru, baba yake alikuwa mwajiriwa na mwanataaluma katika mifugo yaani daktari wa mifugo ilikuwa fani yake na kisha baadae aliamua kuacha utumishi wa umma na kujikita kwenye siasa na mwaka 1956 na alijiunga na TANU, akishika nafasi ya Katibu wa Mkoa.

"TANU ilipozaliwa kulikuwa na wakereketwa wengi kisiasa akiwamo baba, Nyerere, Joseph Nyerere (mdogo wa mwalimu Nyerere), Kissoky na wengine wengi, ambao walijikita katika ukombozi hata kwa nchi za Kusini barani Afrika," alisema.

Stephen alisema PAFMECA, Mwakangale alishiriki harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika na TANU ilipoasisiwa, alichaguliwa na kuonyesha mchango mkubwa kisiasa na harakati hizo zilimfanya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO) mwaka 1957.

Maonyesho ya Nanenane 2023 yanayofanyika kitaifa jijini Mbeya, kwenye viwanja vya John Mwakangale, yalizinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango. Kaulimbiu ya mwaka huu ni; "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula."



# Wananchi wasema hawaifahamu mifuko ya kuwawezesha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya serikali ya kuazisha mifuko ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwamo wajasiriamali kwa bahati mbaya hawaifahamu mifuko hiyo, hatua ambayo imeibua malalamiko kwa walengwa na kushindwa kufaidika nayo.

Akiwasilisha ripoti ya utafiti kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, katika mkutano wa asasi za kiraia uliofanyika visiwani humo, Aisha Haji Ramadhan, kutoka Taasisi ya Milele Foundation, alisema nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwakomboa wananchi wake ikiwamo wajasiriamali ni nzuri kwa kuanzisha mifuko inayotoa mikopo yenye masharti nafuu katika kuendesha biashara zao.

"Wakati umefika kwa mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ifahamike utendaji wake na malengo pamoja na kazi zake ili wananchi walengwa wapate fursa za kufaidika," alisema.

Akizungumza kwa upande wa kundi la vijana, Almasi Mohd Ali kutoka Taasisi ya Zanzibar Youth Forum, alisema wakati umefika kwa vijana kujengewa uwezo katika elimu ikiwamo mitaala ya elimu iliyopo sasa iweze kutoa fursa za kujiajiri wakati wanapomaliza masomo na kuacha tabia ya kusubiri ajira serikalini.

Alisema suala la ajira kwa vijana ni changamoto kubwa na hali hiyo inatokana na vijana wakati wanapomaliza elimu ya juu kuajiriwa serikalini.

"Katika utafiti wetu tumebaini kwamba wakati umefika kwa mitaala ya elimu ya shule na vyuo vikuu kwenda na wakati wa mabadiliko mitaala yake inatakiwa iwawezeshe wanafunzi kujiajiri wakati wanapomaliza masomo tofauti na sasa," alisema.

Kwa upande wa wanawake na uongozi, Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa Ali, alisema bado ushiriki wa wanawake katika vyombo vya kutunga sheria ni mdogo hatua inayochangia sauti zao kusikika katika vyombo vya kutunga sheria.

Alisema katika vyombo vya kutunga sheria ikiwamo Baraza la Wawakilishi, ushiriki wa wanawake ni mdogo wa asilimia 37 na kwa upande wa viongozi wa sheria masheha wapo kwa asilimia 16.

Aidha, alisema wakati umefika kwa wanawake wenyewe kusimama kidete na kujitokeza kugombea nafasi za uongozi ikiwamo katika majimbo ya uchaguzi ili kufikia asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya maamuzi ikiwamo Baraza la Wawakilishi.

"Utafiti wetu umebaini kwamba njia pekee itakayowawezesha wanawake kufikia malengo ya uongozi ni kugombea nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi ambapo itawawezesha kuingia katika vyombo vya maamuzi," alisema.

Wakichangia ripoti hiyo, Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii Zanzibar, Siti Abasi Ali, alisema safari ya Zanzibar ya kufikia usawa wa kijinsia inaendelea na matarajio makubwa kufikia vigezo vilivyofikiwa na nchi kama Rwanda ya asilimia 40 ya wanawake kuingia katika vyombo vya sheria ikiwamo Baraza la Wawakilishi.

Ripoti ya utafiti unaohusisha makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu imetayarishwa na umoja wa asasi za kiraia ikiwemo Juwauza, Tamwa Zanzibar,Jumuiya ya wanasheria wanawake Zanzibar (Zafela) ikiwa na lengo la kujuwa changamoto zinazoyakabili makundi hayo na njia ya kuzipatia ufumbuzi wake.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akivuna miwa katika shamba la darasa la Chuo cha Mafunzo Zanzibar, katika viwanja vya maonyesho ya kilimo Nanenane Zanzibar Kizimbani Dole, Wilaya ya Magharibi "A" Unguja juzi. **PICHA: IKULU**

# Serikali yaongeza bei ya karafuu kuanzia leo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeongeza bei ya zao la karafuu katika msimu huu wa zao hilo ambao inaanza leo Agost 3.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shaban, alisema serikali imeongeza bei za zao hilo kwa mkulima na karafuu daraja la kwanza serikali itanunua Sh. 15,000 kutoka Sh. 14,000 kwa kilo moja.

Alisema karafuu daraja la pili itauzwa kwa Sh. 13,500 badala ya Sh. 13,000 kwa kilo moja, daraja la tatu Sh. 12,500 badala ya Sh. 12,000 kwa kilo moja na daraja la chini (Mpeta) litabaki Sh. 7,000.

Kuhusu mfumo wa malipo, alisema utaratibu wa malipo kwa wakulima utakuwa kwa njia za kielektroki kupitia mifumo ya kibenki na mitandao ya simu, ingawa malipo ya fedha taslim yatafanyika kwa kiwango kidogo cha karafuu (chini ya gunia moja). "Hatua hii ya malipo imechukuliwa kwa ajili ya kulinda usalama wa fedha za kwa wananchi," alisema. Alisema kutokana na umuhimu wa zao la karafuu kwa wananchi na uchumi kwa ujumla, serikali imewataka wananchi kuuza karafuu zote katika Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na kuanika kwa kutumia jamvi ili kupata ubora na daraja la kwanza.

Aidha, aliwataka wakulima wa zao hilo kuzingatia ukaukaji wa karafuu unaostahiki, kuzingatia usafi wa karafuu kabla kupeleka katika vituo vya ununuzi ili kuepuka usumbufu na kuwa na namba za simu zilizosajiliwa kwenye mifumo ya kupokea fedha pamoja na nambari akaunti za benki zilizo hai.

"Wakulima kujiepusha na magendo ya karafuu, na endapo ikibainika mwananchi yeyote kujihusisha na vitendo hivyo, serikali itachukua hatua kwa mujibu wa sheria na kutoa ushirikiano na taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama za utoroshaji wa karafuu," alisema.

Alisema shirika linatoa shukrani kwa wadau wote wakiwamo wakulima wa karafuu, Kikosi Kazi cha kudhibiti magendo ya karafuu, Benki ya Watu wa Zanzibar, Kampuni ya simu ya Tigo/Zantel, waandishi wa habari na wadau wengine ambao wanasaidia katika kufanikisha ununuzi wa karafuu.

## Wananchi waahidiwa pembejeo za kilimo kuwa endelevu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kuwapatia wakulima pembejeo na huduma nyingine za kilimo, ili kuwaondoshea changamoto kuelekea mapinduzi ya kijani kwa uchumi endelevu.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo kwenye ufunguzi wa maonyesho ya Nanenane, yanayoendelea huko Kizimbani, Wilaya ya Magharibi A Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema, serikali inawajibu wa kuwawezesha vijana na wanawake kwenye shughuli zao za kilimo na kuitaka Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuandaa utaratibu mzuri wa kuweka takwimu zao kwa lengo la kuhakikisha inapotoa pembejeo ziwafikie wahusika kwa urahisi na kwa wakati muafaka.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi ameiagiza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuzitengeneza barabara zote zilizomo kwenye viwanja vya Maonesho ya Nanenane Kizimbani, kwa kiwango cha lami ili kuyaongezea hadhi maonesho ya mwakani. Alisema, serikali inawajibu wa kuhakikisha ardhi ndogo ya kilimo ilioyopo inatumika kwa ufanisi ili izalishe na kuongeza tija.

"Umefika wakati tuwe na takwimu sahihi ya ukubwa wa ardhi ya kilimo tuliyonayo ili tuweze kuweka mipango mizuri ya kuitumia," alilisistiza Dk. Mwinyi.

Akizungumzia hali halisi ya uzalishaji kilimo nchini, Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imeweka jitihada mbalimbali kufanikisha sekta hiyo na kueleza kuwa na matokeo yenye tija.

Alisema ongezeko la uzalishaji wa mboga na matunda nchini kutoka tani 64,820 mwaka 2021 hadi tani 66,304 mwaka 2022, muhogo umeongezeka kutoka tani 181,668 mwaka 2021 hadi tani 202,519 mwaka 2022.

Dk. Mwinyi alisema, ongezeko la ng'ombe waliochinjwa kutoka 25,916 mwaka 2021 hadi 27,326 mwaka 2022, kuku waliochinjwa wameongezeka kutoka 751,073 mwaka 2021 hadi 1,130,591 mwaka 2022 na mayai yaliyozalishwa yameongezeka kutoka 15,723,843 mwaka 2021 hadi 21,659,078 mwaka 2022.

Alisema, hizo ni dalili nzuri za mafanikio katika sekta ya Kilimo na Ufugaji kwa Zanzibar.

Pia, lengo la serikali kufanya maonesho ya kilimo ni kuhimiza kufanya mapinduzi ya kilimo kwa kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa mbinu bora za kilimo ikiwemo matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji maji na zana za kisasa kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji kwa mazao ya chakula na biashara ili kupata tija zaidi na kuwapa faida kubwa wakulima na Taifa kwa jumla na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo ili kuendeleza sekta ya kilimo pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi. Aliwasihi vijana kutumia fursa ya maonesho hayo kujifunza zaidi ili wahamasike na kujiajiri kwenye sekta ya kilimo kwa lengo la kuwa na uhakika wa chakula katika kupiga hatua za maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis alisema, wizara inajitahidi kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya serikali katika kuimarisha sekta ya kilimo nchini kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya 145 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025.

Katibu Mkuu Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Seif Shaaban Mwinyi aliwashauri vijana na wanawake kuzitumia fursa zinazopatikana kwenye Mradi wa mashamba makubwa ya pamoja (BBT) ulioanzishwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan ili kujiendeleza kiuchumi na kuyafikia mapinduzi ya kilimo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JUMA MAKAMBA JUMA** natangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya HAOJUE yenye jina la umiliki GS GROUP LIMITED yenye usajili namba MC 828 CEL, CHASSIS NAMBA: LC6PCJK22J0093885 na ENGINE NAMBA : 156FM1-5AD2F50677. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PWA/BAG/RB/19907/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NDENGU RASHIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S2537-0234** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ILALA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/MAG/RB/257267/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSE MIGUEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TATA yenye jina la umiliki HAPPCOR TRADING & HIRE COMPANY LIMITED yenye usajili namba : T991 DMD, CHASSIS NAMBA: MAT386534HSR18960 na ENGINE NAMBA: 497TC93JSY828361.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/212594/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN ANDASON AYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba: MC969 DKT na CHASSIS NAMBA: D3PCK6J2N2003975. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/259609/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAINES SETH MVELA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI **T637 ARV** YOYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA **IRI/IRI/RB/259567/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**CLAVER MOTORS LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **T278 ALU na T 680 AEX**. kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/255821/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JENIPHER MEDSON MWAKYOMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.1141-0030** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SEKONDARI SWILLA MWAKA 2020.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/233097/2023**


***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Donald Trump akabiliwa na mashtaka mengine manne

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump, ameshtakiwa kwa makosa manne ikiwamo kupanga njama ya kubatilisha matokeo ya uchaguzi wa 2020.

Kiongozi huyo, pia anatuhumiwa kula njama ya kulaghai, kuharibu ushahidi na kula njama dhidi ya haki za raia.

Hati hiyo ya mashtaka inahitimisha uchunguzi wa matukio yanayohusu ghasia za Januari 6, 2021 zilizoanzia katika Ikulu ya Marekani.

Trump, mwenye miaka 77, ametia nia ya kuwania tena nafasi ya urais, amekanusha kuhusika na makosa hayo.

Akizungumzia kupitia mitandao ya kijamii, Trump aliitaja kesi hizo kuwa ya kipuuzi.

Tayari anakabiliwa na kesi zingine mbili ambazo ni kutunza vibaya faili zilizoainishwa, na kughushi rekodi za biashara ili kuficha malipo ya pesa aliyofanya kwa nyota wa filamu za ngono.

Uchunguzi huo umezingatia hatua za Trump katika kipindi cha miezi miwili na kushindwa kwake kuzuia ghasia zilizotokea Washington DC, wakati wafuasi wake walipovamia jengo la bunge la Congress kupinga kuidhinisha ushindi wa Rais Joe Biden wa chama cha Democratic.


Kiongozi wa uchunguzi huo, wakili maalum aliyeteuliwa na idara ya sheria ya Marekani Jack Smith, alisema juzi kuwa kulikuwepo na shambulio dhidi ya mji mkuu wa taifa hilo Januari 6, 2021 na kulitaja kama shambulio ambalo halijawahi kushuhudiwa dhidi ya demokrasia ya nchi hiyo.

Wakili Smith alimalizia taarifa yake fupi kwa kuahidi mchakato wa kushtakiwa haraka kwa kiongozi huyo, huku akisisitiza kwamba rais huyo wa zamani lazima sasa achukuliwe kuwa hana hatia hadi ithibitishwe.

Trump anatarajiwa kufika mahakamani leo mjini Washington DC, kujibu mashtaka hayo mahakamani.

Hati ya mashtaka yenye kurasa 45 iliorodhesha washiriki sita ambao hawakutajwa majina: mawakili wanne, afisa wa idara ya haki na mshauri wa kisiasa.

Hati hiyo ya mahakama ilimshutumu Trump kwa kufanya njama ya kudhoofisha, kuzuia, na kushindwa kwa kazi ya serikali kuu kupitia ukosefu wa uaminifu, ulaghai na udanganyifu. **BBC**



Vikosi vya zimamoto vikichunguza jengo la ghorofa lililoshambuliwa na ndege isiyo na rubani mjini Moscow jana. **PICHA: IMAGO**

# Ulaya yaanza kuhamisha raia wake Niger

**ROMA, Italia**

NCHI mbalimbali za Ulaya zimewahamisha raia wao kutoka nchini Niger baada ya siku chache kufanyika mapinduzi ya kijeshi.

Ufaransa ilianza kuwahamisha raia wake kutoka nchini himo huku kukiwa na chuki dhidi raia wake kufuatia wananchi kuyaunga mkono mapinduzi hayo.

Mapinduzi hayo yamesababisha maandamano dhidi ya utawala wa kikoloni wa zamani, huku ubalozi wa Ufaransa ukishambuliwa.

Hata hivyo, Ufaransa ilisema haina mpango wa kuwarejesha nyumbani takribani wanajeshi 1,000 wa nchi yake walioko Niger kama sehemu ya juhudi za kukabiliana na wanamgambo wa Kiislamu.

Ujerumani imewataka raia wake kuchukua ofa ya Ufaransa kusaidia kuondoka nchini humo.

Italia nayo imewasafirisha watu 87 hadi mjini Roma jana.

Ndege hiyo ilikuwa imebeba Waitaliano 36, Wamarekani 21 na Mwingereza mmoja, kulingana na shirika la habari la Reuters.

Mataifa ya Burkina Faso na Mali, yameonya endapo litafanyika jaribio lolote la nguvu la kumrejesha madarakani rais aliyepinduliwa litaonekana kama tangazo la vita.

Majirani hao wawili, pia walitawaliwa na Ufaransa, wote wameachana kihusiano na nchi hiyo na kumkumbatia Russia, baada ya kufanya mapinduzi yao wenyewe katika miaka ya hivi karibuni.

Onyo lao linaashiria kuwepo kwa mabadiliko makubwa yanayoweza kuzidisha hali tete katika eneo hilo linalohangaika na wapiganaji wa Kiislamu.

Niger, ambayo ina utajiri mkubwa wa madini ya uranium, imekuwa mshirika mkuu wa Magharibi katika vita dhidi ya itikadi kali za kijihadi katika eneo la Sahel.

Ufaransa na Marekani zina kambi za kijeshi katika nchi hiyo.

Baada ya viongozi wa kijeshi wa Mali kuchagua kushirikiana na mamlaka ya Wagner wa Russia mwaka 2021, Ufaransa ilihamisha kitovu cha operesheni zake za kikanda za kukabiliana na ugaidi hadi nchini Niger.

**BBC**

# Mji wa Moscow washambuliwa

**MOSCOW, Russia**

RUSSIA imekabiliwa na mashambulizi kadhaa ya ndege zisizo na rubani katika mji mkuu Moscow na majengo kadhaa yamelengwa.

Ikulu ya Kremlin iilisema hatua kadhaa zimechukuliwa kuboresha ulinzi katika mji huo mkuu.

Jengo la ghorofa linalotumika na wizara tatu, limeshambuliwa jana ikiwa ni mara ya pili katika kipindi cha siku mbili zilizopita.

Russia imeishutumu Ukraine kwa mashambulizi hayo katika ardhi yake.

Maofisa wa Russia wamedai hatua ya Ukraine kuzidisha mashambulizi katika mji wa Moscow inaonesha kushindwa kwake katika mpango wake wa kuchukua udhibiti wa maeneo yaliyonyakuliwa na Russia.

Wiki iliyopita ya Rais wa UkraineVolodymyr Zelensky alisema taratibu vita vinarejea ndani ya Russia.

Mshauri wa Zelensky, Mykhailo Podolyak, ameandika kwenye ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Twiter kwamba Russia imeanza sasa kuzoea matokeo ya vita kamili bila kuthibitisha au kukana kuhusika kwa nchi yake katika mashambulizi hilo.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, ilisema itatekeleza jukumu lake na kuchukua hatua zaidi za ulinzi kufuatia shambulio hilo jipya la ndege isiyo na rubani katika mji wa Moscow. Msemaji wa Ikulu wa Kremlin Dmitry Peskov, alikiri kuwepo hatari ya mashambulizi zaidi.

Mashambulizi ya mara kwa mara ya ndege zisizo na rubani katika ardhi ya Russia yadhihirisha udhaifu wa nchi hiyo wakati ikiendelea na uvamizi wake nchini Ukraine ukiingia mwezi wa 18.

Katika hatua nyingine, Wizara ya ulinzi ya Russia ilisema kuwa imezuia mashambulizi kadhaa ya ndege zisizo na rubani za Ukraine yaliyokuwa yakilenga meli zake za kiraia na zile za jeshi la wanamaji katika Bahari Nyeusi.

Wizara hiyo ilibaini kuwa meli hizo mbili zilikuwa katika harakati ya kudhibiti usafirishaji katika bahari ya kusinimagharibi mwa Sevastopol.

**Maofisa wa Russia wamedai hatua ya Ukraine kuzidisha mashambulizi katika mji wa Moscow inaonesha kushindwa kwake katika mpango wake wa kuchukua udhibiti wa maeneo yaliyonyakuliwa na Russia.**

HABARI MICHEZO

# MBOMBO: KAMBI TUNISIA IMETUIMARISHA, AJE YEYOTE

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Azam FC, Indriss Mbombo amesema kambi ya nchini Tunisia imewafanya kuwa vizuri na kuimarika na kwa sasa wapo tayari kucheza na timu yoyote na kupata matokeo mazuri katika msimu mpya wa ligi na mashindano ya kimataifa 2023/2024.

Kikosi cha Azam FC, kilirejea juzi Dar es Salaam kikitokea Tunisia ambako waliweka kambi ya wiki tatu kujiandaa na msimu mpya na sasa wamerejea kivingine.

Azam FC Agosti 9, watacheza mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga kwenye uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Akizungumza na Nipashe jana, Mbombo alisema kambi ya Tunisia imewasaidia kupata muda wa kufahamiana na wachezaji wapya jambo ambalo limewatengenezea muunganiko mzuri katika kikosi chao.

Alisema wamepata mafuzo mazuri kutoka kwa kocha Youssouph Dabo ambaye amepata muda wa kuwaandaa wachezaji wake na wako tayari kiufundi, mbinu na utimamu wa mwili kucheza mechi na timu yoyote.

"Tumefanya mazoezi mazuri, kocha Dabo amepata muda wa kunoa kikosi kwa muda mrefu, ameona mapungufu na kufanyia kazi, kikubwa kazi yetu ni kupambana na kutafuta matokeo chanya kwa kila mechi."

"Tayari kocha ameshafanya majukumu yake, na kikubwa tuko tayari kwa msimu mpya na kuleta ushindani mkubwa," alisema Mbombo.

Aliongeza kuwa wamerejea kivingine kuleta ushindani katika ligi kwa kufikia malengo yao ya kutwaa mataji yote ikiwemo kombe la Ngao ya Jamii, wakitarajia kucheza na Yanga SC.

Kikosi cha Azam FC kipo kambini na watakuwa na michezo miwili ya kimataifa ya kirafiki watacheza Jumamosi dhidi ya Bandari FC katika uwanja wa Azam Complex, Chamazi.



Wanafunzi wa Shule ya msingi Gerezani, wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtibwa yawakaushia wageni

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya Mtibwa Sugar umeweka wazi kuwa hawana mpango wa kusajili wachezaji wa kigeni na msimu huu watawatumia wachezaji wazawa pekee kwenye ligi kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo Thobias Kifaru alisema msimu huu watadili na wazawa pekee baada ya kuona wageni kutowasaidia.

"Msimu uliopita tulisajili wachezaji wa kigeni lakini ukweli hawakutusaidia, tulikuwa na hali mbaya na hatutaki kufanya makosa mengine msimu ujao," alisema Kifaru.

Alisema wanaamini kama wachezaji wazawa watapata maandalizi mazuri na wanaweza wakaisaidia timu hiyo kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita.

"Msimu uliopita tuliponea chupu chupu tushuke daraja kutokana na changamoto za wachezaji wa kigeni ambazo zilichangia kwa kiasi kikubwa sisi kufanya vibaya, msimu huu tunarudisha imani yetu kwa wachezaji wa ndani na tunaamini mambo yatakuwa mazuri," alisema.

Msimu uliopita Mtibwa ilimaliza ligi ikiwa kwenye nafasi ya 10 kwa kukusanya pointi 35 pekee.

## JKT Queens kuweka kambi Bukoba

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya soka ya wanawake ya JKT Queens kitaingia kambini kuanzia Agosti 5 Wilayani Bukoba Mkoa wa Kagera kujiandaa na michuano ya wanawake ya Baraza la Vyama vya Michezo Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) itakayoanza Agosti 12 nchini Uganda.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, mwenyekiti wa timu hiyo Meja Ester Rioba alisema lengo la kuweka kambi mkoani humo ni kuzoea hali ya hewa ya ambayo inalingana na Uganda.

"Maandalizi yanaendelea vyema, Agosti 5 tutaanza kambi yetu Bukoba, malengo ya timu ni kuona tunafanya vizuri kwenye mashindano ya CECAFA na kuitangaza vyema nchi yetu," alisema Meja Rioba.

Alisema wanafahamu wakifanya vizuri mashindano hayo ya CECAFA watapata nafasi ya kushiriki mashindano ya Afrika kwa vilabu vya soka vya wanawake.

"Kote huko tunataka tufanye vizuri, lakini lazima tuanzie kwanza kwenye mashindano haya ya Afrika Mashariki na Kati, tumejipanga kwa kweli," alisema Meja Rioba.

## Arusha kusaka wanariadha mkoa Agosti 25

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha riadha Mkoa wa Arusha (ARAA) kimeandaa mashindano ya mchezo huo yatakayofanyika kwenye uwanja wa Sheikhe Amri Abeid Agosti 25 yakiwa na lengo la kusaka wachezaji watakaowakilisha mkoa huo kwenye mashindano ya taifa.

Mashindano ya taifa ya mchezo huo yamepangwa kufanyika mkoani Morogoro kwa siku mbili yakianza Septemba 8-9.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana kutoka mkoani humo, Katibu Mkuu wa ARAA Rogath John, alisema Arusha imejipanga kufanya vizuri kwenye mashindano hayo ya taifa na mashindano wanayoyoandaa ni mahususi kwa ajili ya kupata wanariadha wenye viwango vikubwa.

"Mashindano haya tunayoyaandaa yatatusaidia kupata kikosi cha wachezaji 30 watakaokwenda kushiriki mashindano ya Taifa Morogoro, tutaka kufanya vizuri ndio maana tutanaka kuyatumia haya mashindano yetu kupata wanariadha bora," alisema John. Aidha, alisema maandalizi yanaendelea vizuri kuelekea katika mashindano hayo ya Arusha na wanariadha waliojiandikisha kushiriki wana morali na hamasa kubwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RAYA SANA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imefikia makubaliano na Brentford kwa ajili ya mlinda lango David Raya mwenye umri wa miaka 27, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania akikadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 40. **(Evening Standard)**

### DOKU AWANIWA

MANCHESTER City inamtaka winga wa Rennes kutoka Ubelgiji, Jeremy Doku, huku klabu hiyo ikimtazama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kama mbadala wa Riyad Mahrez, ambaye alijiunga na Al-Ahli ya Saudi wiki iliyopita. **(Fabrizio Romano)**

### OLISE ATAKIWA CITY

MANCHESTER City pia inamwona mshambuliaji wa Crystal Palace, Michael Olise mwenye umri wa miaka 21 kama chaguo la kuchukua nafasi ya Riyad Mahrez, huku kocha wa Palace Roy Hodgson akikiri kuwa itakuwa vigumu kumbakisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa chini ya miaka 21 katika klabu hiyo msimu huu. **(Athletic)**

### DAU LAKATALIWA

DAU la Bayern Munich la pauni milioni 85 kumnunua mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane limekataliwa, huku Spurs wakitaka zaidi ya pauni milioni 100 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. **(Independent)**

### KANE NA BAYERN

HARRY Kane anatarajia kusalia Tottenham msimu huu ikiwa klabu hiyo haitaafikiana na Bayern kabla ya mechi ya kwanza ya Ligi Kuu dhidi ya Brentford, kwani anaamini itakuwa si haki kuondoka baada ya kuanza kwa msimu mpya. **(Evening Standard)**

### ADAMS, ALVAREZ WAWANIWA

CHELSEA wamewaongeza kiungo wa kati wa Leeds United na Marekani, Tyler Adams mwenye umri wa miaka 24 na kiungo wa kati wa Ajax na Mexico, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 25 kwenye orodha ya wachezaji wanaopania kuwanunua. **(Times)**

### COLWILL KUSAINI

MLINZI wa timu ya taifa ya England chini ya umri wa miaka 21, Levi Colwill amekaribia kusaini mkataba mpya Chelsea. **(TalkSPORT)**

### EVANS MKATABA MPYA

BKI wa Ireland Kaskazini, Jonny Evans mwenye umri wa miaka 35 anatazamiwa kupewa mkataba mpya wa mwaka mmoja na Manchester United baada ya kujiunga na klabu hiyo kwa muda mfupi msimu huu. **(Belfast Telegraph)**

### DEMBELE NA PSG

KLABU ya Paris St-Germain imeanzisha kipengele cha kutolewa cha euro milioni 50 kumsajili winga wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 26. **(Fabrizio Romano)**

### JAMES BASI TENA

WEST Ham imeachana na mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Southampton, James Ward-Prowse, wakiamini kwamba thamani ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 iko juu sana. **(Sky Sports)**

### BORGES KUTUA AJAX

WINGA wa Manchester City, Mreno Carlos Borges mwenye umri wa miaka 19, anakaribia kujiunga na Ajax kwa mkataba wa thamani ya euro milioni 20. **(Athletic)**

DO… A SOKA
MA… A ULAYA



# XAVI ASIKITISHWA NA UHAMISHO WA DEMBELE

**Kocha huyo amethibitisha mshambuliaji huyo amemwambia anataka kuondoka kwenda kujiunga na…**

**LAS VEGAS, Marekani**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi Hernandez amesema amesikitishwa na Ousmane Dembele baada ya kuthibitisha kuwa fowadi huyo amemwambia anataka kujiunga na Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa ESPN.

Barca na PSG wamebakia kwenye mazungumzo kuhusu ada ambayo inatarajiwa kuwa karibu euro milioni 50, na uhamisho huo huenda ukakamilika siku chache zijazo.

"Nimesikitishwa kidogo," alisema Xavi akiiambia televisheni ya Katalunya baada ya timu yake kushinda 1-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya AC Milan huko Las Vegas nchini Marekani, Jumanne.

"Ametuambia kwamba anataka kwenda PSG. Tulijaribu kumbakisha, lakini hakuna tunachoweza kufanya. Aliniambia tayari amezungumza na kocha wa PSG, Luis Enrique na Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi. "Hakukuwa na njia ya kumshawishi, huu ni uamuzi wa mwisho na ni uamuzi wake binafsi. PSG wametoa ofa kubwa na hatuwezi kushindana nayo."

Majeraha yamekuwa tatizo kubwa kwa Dembele ndani ya Barcelona tangu alipowasili katika klabu hiyo akitokea Borussia Dortmund mwaka 2017.

Dembele mwenye umri wa miaka 26 alionekana kuondoka Barca mwaka 2022, huku mkurugenzi wa michezo, Mateu Alemany akimwambia atafute klabu mpya wakati huo, lakini nia ya Xavi ya kumbakisha katika klabu hiyo ilimfanya asaini mkataba mpya msimu uliopita.

Lakini mkataba huo wa miaka miwili, ambao unaisha mwaka 2024, unajumuisha kifungu cha kutolewa cha euro 50 milioni ambacho kilikuwa halali hadi Julai 31.

Kifungu hicho kiliongezeka mara mbili hadi euro milioni 100 Jumatatu baada ya makubaliano ya awali kumalizika.

"Ni aibu, tulikuwa tumemtunza sana kuhakikisha anafurahi hapa," aliongeza Xavi aliongeza katika mkutano na waaandishi wa habari alipoulizwa ni kiasi gani aliwekeza kwa Dembele.

"Nilijua yote kuhusu kifungu hicho. Alemany na mimi tumekuwa pamoja mchana na usiku na tulijua kuna nafasi angeenda. Lakini alionekana kuwa na furaha kwangu. Sikutarajia lakini imetokea.

"Mwisho wa siku, ni hali ambayo tumejitayarisha na sasa tunapaswa kuimarisha kwa sababu inatudhoofisha."

Dembele alijiunga na Barca kutoka Borussia Dortmund mwaka 2017 kwa ada ya awali ya euro milioni 105.

Majeraha yamekatiza muda wake katika klabu hiyo na kumfanya acheze mechi 185 katika michuano yote ambapo amefunga mabao 40.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,139,8

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 03 AGOSTI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/08/23 | 17:00 | Tobol Kostanay vs FC Basel | 3.10 | 3.40 | 2.16 |
| 02. 03/08/23 | 18:00 | Pyunik Yerevan vs Kalmar | 2.31 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 03/08/23 | 18:00 | Santa Coloma vs Sutjeska | 2.80 | 3.40 | 2.33 |
| 04. 03/08/23 | 19:00 | Urartu vs Farul Constanta | 2.51 | 3.21 | 2.71 |
| 05. 03/08/23 | 19:00 | FK Panevezys vs Hapoel Beer Sheva | 3.06 | 3.36 | 2.20 |
| 06. 03/08/23 | 19:45 | Zalaegerszegi TE vs NK Osijek | 2.51 | 3.27 | 2.66 |
| 07. 03/08/23 | 20:00 | Sepsi Osk vs CSKA Sofia | 2.71 | 3.21 | 2.51 |
| 08. 03/08/23 | 20:00 | Dila Gori vs Vorskla Poltava | 2.35 | 3.35 | 2.80 |
| 09. 03/08/23 | 21:00 | Vojvodina vs Apoel Nicosia | 2.75 | 3.25 | 2.44 |
| 10. 03/08/23 | 21:00 | Aarhus vs Brugge | 3.10 | 3.25 | 2.22 |
| 11. 03/08/23 | 21:30 | Larne vs KF Ballkani | 2.65 | 3.39 | 2.46 |
| 12. 03/08/23 | 21:45 | FC Luzern vs Djurgardens IF | 2.11 | 3.40 | 3.20 |
| 13. 03/08/23 | 22:00 | Shamrock Rovers vs Ferencvaros TC | 3.05 | 3.30 | 2.23 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP AITAKA UEFA, FIFA KUINGILIA USAJILI WA SAUDIA

**LONDON, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp ametoa wito kwa Shirikisho la soka Duniani, FIFA, na lile la Ulaya, UEFA, "kutafuta suluhu" kuhusu kufunga dirisha la uhamisho la Saudi Arabia mapema.

Dirisha la majira ya joto kwa ligi tano bora za Ulaya litafungwa Septemba Mosi, lakini klabu za Ligi Kuu ya Saudia, Saudi Pro League, zinaweza kusajili wachezaji hadi Septemba 20.

Liverpool imewaona Roberto Firmino, Jordan Henderson na Fabinho wakiondoka Anfield kuelekea Saudi Arabia, na Klopp alisema klabu za Ulaya zinahitaji msaada zaidi.

Alipoulizwa kuhusu ushawishi wa Saudia, Klopp aliuambia mkutano wake na waandishi wa habari Jumanne: "Ni mkubwa, kwa sasa.

Jambo baya zaidi ninalofikiri ni kwamba dirisha la uhamisho nchini Saudi Arabia litaendelea kuwa wazi kwa wiki tatu zaidi".

"UEFA au FIFA lazima itafute suluhu kwa hilo. Lakini mwisho, kwa wakati huu, sijui nini hasa kitatokea."

Hivi karibuni kocha wa Manchester City, Pep Guardiola alionya kuwa Saudi Arabia imebadilisha soko baada ya kuondoka kwa Riyad Mahrez kwenda Al Ahli.

Klopp pia alikanusha ripoti zinazomhusisha nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappé kuhamia Anfield msimu huu wa joto.

"Tunacheka," Klopp aliiambia Sky. "Naweza kusema kwamba nadhani ni mchezaji mzuri sana, lakini hali ya kifedha haitufai hata kidogo.

"Nisingependa kuharibu hadithi sasa ... lakini nijuavyo, hakuna chochote.

"Inawezekana kwamba mtu mwingine kutoka klabu anaandaa kitu na anataka kunishangaza ... hilo halijafanyika kwa miaka minane ambayo nimekuwa hapa. Hiyo itakuwa mara ya kwanza."



# Martínez ahimiza wachezaji kuzomeana

**LAS VEGAS, Marekani**

LISANDRO Martínez amewahimiza wachezaji wenzake wa Manchester United kuendelea kuzomeana baada ya André Onana kunaswa akimtusi Harry Maguire wakati wa kipigo kutoka kwa Borussia Dortmund.

Onana alikimbia nje ya lango lake na kumzomea Maguire baada ya beki huyo wa England kufanya makosa wakati wa kichapo cha 3-2 huko Las Vegas nchini Marekani Jumapili.

Lakini Martínez alisema ni jambo zuri na anataka kuliona mara nyingi zaidi msimu huu.

"Ni bora kwa hilo," alisema Martínez, baada ya kuulizwa kuhusu tukio lililohusisha Maguire na Onana.

"Ikiwa una umakini, unaweza kupigana na wachezaji wenzako pia, unahitaji kuhakikisha kuwa kila mtu yuko mkali, lakini hakuna kilichotokea. Ni sehemu ya mpira wa miguu."

Martínez anamfahamu Onana vyema tangu walipokuwa pamoja Ajax. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Cameroon amewasili kutoka Inter Milan kuchukua mikoba ya David de Gea, ambaye aliihama klabu hiyo akiwa mchezaji huru msimu huu wa joto.

"Ana utu mkubwa," aliongeza Martínez. "Anaweza kucheza mpira wa miguu, anaweza kukabiliana na shinikizo, ana maoni chanya, ni kiongozi, hiyo ndiyo staili ya Manchester United."

Martínez amerejea kucheza tena baada ya kukosa mwisho wa msimu uliopita kutokana na jeraha la mguu.

Muargentina huyo hajapunguza mbinu yake ya ukali wakati wa maandalizi ya msimu mpya na alikuwa akizozana na Martin Ødegaard wa Arsenal na Jude Bellingham wa Real Madrid.

"Ninapocheza soka, natoa kila kitu," alisema. "Nacheza hivi, kwa shauku kwa sababu nikiangalia beji, naiwakilisha klabu hii, inashangaza, ninachoweza kutoa ni mwili wangu na moyo wangu na kila kitu. Ninaiwakilisha klabu hii kwa kila kitu na natumaini wachezaji wote hufanya hivyo.

"Ninajihisi fiti kabisa sasa, najisikia furaha kwa sababu napenda soka. Ilikuwa ngumu sana ukiwa nje na huwezi kufanya lolote, unajua? Lakini sasa niko tayari na ninatazamia kuwa na wakati mzuri zaidi."

359,317/-

# ROBERTINHO AKIRI ANA WAKATI MGUMU

**Na Saada Akida**

BAADA ya kurejea nchini jana alfajiri wakitokea Uturuki, Kocha wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema kwa sasa ana wakati mgumu wa kupanga kikosi kutokana na ubora wa wachezaji wake kwa sasa.

Robertinho alisema katika kila namba ana wachezaji ambao kwa sasa uwezo wao unafanana hivyo itamlazimu kutuliza kichwa kujua nani wa kuanza katika mchezo husika.

"Naipongeza klabu ya Simba, Rais wa Heshima, na watendaji wengine kwa kazi waliyoifanya, kwa sababu sasa tuna uwiano mzuri wa kufanya mabadiliko ya wachezaji tunapopata majeruhi kwenye kikosi cha kwanza, kwa sasa naona kazi kubwa ipo kwangu katika kuamua nani aanze kwenye mchezo," alisema Robertinho.

Alisema uimara wa wachezaji wake umetokana na maandalizi mazuri waliyoyafanya na wanayoendelea kuyafanya kuelekea kwenye msimu mpya wa ligi kuu.

"Kambi ya Uturuki ilikuwa bora sana kwetu, imewaimarisha wachezaji na imewapa nafasi ya kuzoeana..., kwa sasa yamabeki mambo machache sana ya kiufundi ambayo naamini mpaka tunaanza ligi yatakuwa sawa," alisema Robertinho

Alisema kwa sasa wanajiandaa na mchezo wao wa Ngao ya jamii dhidi ya Singida Fountain Gate utakaochezwa Agosti 10 kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

"Lakini kabla ya Ngao ya Jamii tutakuwa na mchezo wa kirafiki siku ya tamasha la Simba 'SimbaDay', huo pia ni muhimu kwetu kwenye maandalizi, lakini ni sehemu ambayo mashabiki wetu wataiona timu yao kwa mara ya kwanza tangu tutoke Uturuki," alisema Robertinho.

Simba walikuwa kambini Uturuki kujiandaa na msimu mpya wa 2023/24 ambapo wamerejea juzi tayari kwa ajili ya tamasha la Simba Day litakalofanyika Jumapili ijayo kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

# UWEKEZAJI SIMBA SC

INATOKA UK. 24

likamilisha kwa kubariki mchakato huo na kuwapa masharti na majukumu ya kufanya, hivyo suala hilo kwao lilishaondoka.

"Sisi na Simba suala letu tulilifunga kwa sababu walikuja wakapewa masharti, kuna majukumu yaliyokuwa ya mwekezaji na majukumu yaliyokuwa ya Simba yenyewe, sasa ilipoletwa baada ya vigezo kukamilika tulitoa cheti cha ruhusa kuwa muungano ule umepitishwa kile kilichokuwa kimeombwa kimeridhiwa baada ya hapo kilichobaki kwao ni utekelezaji tu," alisema Erio.

Aidha, alipotafutwa Mwenyekiti wa klabu ya Simba ambaye anaingia kwenye vikao vya bodi ya klabu hiyo akiwakilisha upande wa wanachama, alisema FCC wako sahihi kueleza wapi mchakato huu ulipokwamia na wametusaidia sisi kufahamu.

"Nadhani katika hili watafuteni wazee wa Baraza la Wadhamini wao wanaweza kukwambieni zaidi tatizo ni nini, mimi binafsi sina la kuongea, FCC wameshawaambieni hivyo," alisema Mangungu.

Mchakato wa mabadiliko ndani ya klabu ya Simba ulioanza mwaka 2017 umeonekana kuchukua muda mrefu na mara kwa mara kumekuwa kunaibuka sintofahamu, huku wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wakiwa hawajui haswa ni kitu gani, wapi au nani anakwambisha mchakato huo usikamilike.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya vijana wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mshambuliaji Yanga aomba muda

INATOKA UK. 24

huyo wa zamani wa Yanga aliyejiunga na Pyramids ya Misri.

"Klabu ina malengo yake, sisi kazi yetu kama wachezaji ni kusaidia kuyafikia, nafahamu mtangulizi wangu kwenye nafasi hii alifanya vizuri sana na kuchangia mafanikio ya klabu msimu uliopita, nami kwa kushirikiana na wachezaji wengine tutapambana kuhakikisha tunafikia hayo malengo," alisema Konkoni.

Mayele ameondoka ndani ya yanga akiwa mfungaji bora na muhimili wa timu hiyo kwenye mafanikio ya msimu uliopita ambapo Yanga mbali na kutwaa ubingwa wa ligi kuu na kombe la FA, pia ilifika hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/23 | 13:00 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama Marinos | 2.23 | 3.35 | 2.70 |
| 02. 06/08/23 | 13:00 | Kyoto Sanga FC vs Kashiwa Reysol | 2.22 | 3.05 | 2.90 |
| 03. 06/08/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.40 | 3.00 | 2.70 |
| 04. 06/08/23 | 13:00 | Thespakusatsu vs Tochigi SC | 2.75 | 2.90 | 2.45 |
| 05. 06/08/23 | 13:00 | Omiya Ardija vs Blaublitz Akita | 2.65 | 2.95 | 2.46 |
| 06. 06/08/23 | 13:00 | Tokushima Vortis vs JEF United Ichihara Chiba | 2.85 | 3.05 | 2.27 |
| 07. 06/08/23 | 14:30 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.90 | 3.70 | 2.16 |
| 08. 06/08/23 | 14:30 | 1 FC Nuremberg vs Hannover 96 | 2.16 | 3.55 | 3.00 |
| 09. 06/08/23 | 14:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 10. 06/08/23 | 16:00 | Kalmar FF vs AIK | 2.55 | 3.00 | 2.55 |
| 11. 06/08/23 | 16:00 | FK Teplice vs FK Jablonec | 2.60 | 3.20 | 2.37 |
| 12. 06/08/23 | 17:30 | Grasshopper Club Zurich vs FC Basel 1893 | 2.75 | 3.45 | 2.16 |
| 13. 06/08/23 | 18:00 | FK Haugesund vs Rosenborg BK | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 14. 06/08/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.27 | 3.25 | 2.70 |
| 15. 06/08/23 | 18:00 | Blau-Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 16. 06/08/23 | 19:00 | Sunderland AFC vs Ipswich Town | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 17. 06/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.40 | 2.33 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 03/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1242 | South Korea W vs Germany W | 11.17 | 5.69 | 1.20 |
| 13:00 | 3630 | Morocco W vs Colombia W | 6.11 | 3.72 | 1.50 |
| 16:00 | 4140 | CR Belouizdad vs Al Kuwait SC | 2.03 | 3.15 | 3.45 |
| 16:00 | 4620 | AL Wahda Scc (UAE) vs Raja Casablanca | 3.10 | 3.10 | 2.30 |
| 17:00 | 2265 | Tobol Kostanay vs FC Basel | 3.20 | 3.40 | 2.11 |
| 18:00 | 1348 | Al Shabab Riyadh vs US Monastir | 1.22 | 5.69 | 9.81 |
| 18:00 | 2401 | Al Ahly Cairo vs Al Masry Club | 1.69 | 3.37 | 4.70 |
| 18:00 | 3197 | Zamalek vs Al Nasr Riyadh | 3.23 | 3.18 | 2.10 |
| 18:00 | 3729 | Pyunik Yerevan vs Kalmar | 2.35 | 3.24 | 2.89 |
| 18:30 | 4412 | Spartak Trnava vs FK Auda | 1.30 | 5.00 | 9.00 |
| 19:00 | 1441 | Sampdoria vs Virtus Entella | 1.44 | 4.17 | 6.11 |
| 19:00 | 1492 | Urartu vs Farul Constanta | 2.30 | 3.20 | 3.00 |
| 19:00 | 2683 | Dinamo Tbilisi vs Hamrun Spartans | 1.57 | 3.80 | 5.59 |
| 19:00 | 3813 | Zalgiris Kaunas vs Lech Poznan | 5.20 | 4.00 | 1.57 |
| 19:00 | 3848 | FK Panevezys vs Hapoel Beer Sheva | 3.00 | 3.34 | 2.24 |
| 19:00 | 4910 | Sabah vs Rigas Futbola Skola | 1.96 | 3.39 | 3.64 |
| 19:00 | 5956 | Aktobe vs Torpedo Kutaisi | 1.61 | 3.75 | 5.20 |
| 19:45 | 5169 | Zalaegerszegi TE vs NK Osijek | 2.45 | 3.25 | 2.75 |
| 20:00 | 1831 | FC Riga vs Kecskemeti TE | 1.78 | 3.51 | 4.31 |
| 20:00 | 2389 | Neftchi Baku vs Zeljeznicar | 1.90 | 3.45 | 3.80 |
| 20:00 | 2775 | Rosenborg vs Crusaders Belfast | 1.28 | 5.21 | 9.22 |
| 20:00 | 2843 | Levski Sofia vs Shkupi Skopje | 1.48 | 4.01 | 6.41 |
| 20:00 | 3638 | Petrocub vs Maccabi Tel Aviv | 5.79 | 4.09 | 1.51 |
| 20:00 | 3649 | Sepsi Osk vs CSKA Sofia | 2.80 | 3.10 | 2.49 |
| 20:00 | 4310 | Omonia Nicosia vs Gabala | 1.52 | 4.00 | 5.80 |
| 20:00 | 5735 | Dila Gori vs Vorskla Poltava | 2.42 | 3.30 | 2.75 |
| 20:05 | 5744 | Bohemians vs Bodo Glimt | 3.89 | 3.75 | 1.80 |
| 20:30 | 1839 | Progres vs Midtjylland | 5.19 | 4.29 | 1.53 |
| 20:30 | 4579 | Beitar Jerusalem vs PAOK | 3.95 | 3.50 | 1.85 |
| 21:00 | 1886 | KF Drita vs Viktoria Plzen | 6.80 | 4.10 | 1.45 |
| 21:00 | 3131 | Aarhus vs Brugge | 2.95 | 3.25 | 2.31 |
| 21:00 | 3287 | Adana Demirspor vs CFR Cluj | 1.65 | 3.85 | 4.69 |
| 21:00 | 3474 | MSK Zilina vs KAA Gent | 5.99 | 4.59 | 1.44 |
| 21:00 | 3957 | Vojvodina vs Apoel Nicosia | 2.85 | 3.21 | 2.39 |
| 21:00 | 5801 | Hammarby vs Twente | 4.31 | 3.40 | 1.80 |
| 21:00 | 5810 | KF Tirana vs Besiktas | 5.84 | 4.05 | 1.51 |
| 21:15 | 1171 | Aris Salonica vs Ararat Armenia | 1.36 | 4.60 | 7.81 |
| 21:15 | 1396 | HNK Rijeka vs KF Dukagjini | 1.17 | 6.59 | 13.97 |
| 21:15 | 3747 | Hibernian vs Inter Club De Escaldes | 1.20 | 6.40 | 11.01 |
| 21:30 | 1763 | Larne vs KF Ballkani | 2.71 | 3.36 | 2.42 |
| 21:30 | 2542 | Steaua Bucuresti vs CSKA 1948 | 1.66 | 3.60 | 5.00 |
| 21:30 | 3567 | Maribor vs Differdange | 1.34 | 4.89 | 7.79 |
| 21:30 | 5627 | Borac Banja Luka vs Austria Vienna | 4.01 | 3.51 | 1.83 |
| 21:45 | 2927 | FC Luzern vs Djurgardens IF | 2.14 | 3.56 | 3.01 |
| 21:45 | 5766 | Haverfordwest vs B36 Torshavn | 3.05 | 3.45 | 2.16 |
| 21:45 | 5860 | Dundalk FC vs KA Akureyri | 1.76 | 3.75 | 4.10 |
| 22:00 | 1536 | Debreceni VSC vs Alashkert Martuni | 1.63 | 3.79 | 4.98 |
| 22:00 | 5504 | Legia Warszawa vs Ordabasy | 1.38 | 4.49 | 7.59 |
| 22:00 | 5986 | Shamrock Rovers vs Ferencvaros TC | 2.85 | 3.35 | 2.32 |
| 22:15 | 2063 | Vitoria Guimaraes vs NK Celje | 1.41 | 4.41 | 6.82 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Agosti 3, 2023
Nipashe



## Xavi asikitishwa uhamisho wa Dembele

UKURASA 21



Beki wa kushoto wa Singida Fountain Gate, Gadiel Michael (kulia) akijaribu kumtoka mchezaji wa As Vita wakati wa mchezo wa kimataifa wa kirafiki uliochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Liti mjini Singida kuadhimisha kilele cha tamasha la klabu hiyo 'Singida Big Day', kwenye mchezo huo Singida ilishinda mabao 2-1. **PICHA: SINGIDA FG**

### UWEKEZAJI SIMBA

# FCC YASEMA MO DEWJI HANA SHIDA, WANACHAMA TATIZO

●●●Yaeleza mwekezaji amekamilisha taratibu alizotakiwa kuzikamilisha, tatizo lipo upande wa....

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Ushindani wa Biashara (FCC), imesema suala la uwekezaji wa klabu ya Simba tatizo lipo kwa upande wa wanachama wa klabu hiyo na si muwekezaji Mohamed Dewji 'Mo'.

Tume hiyo ilisema kila upande ulipewa majukumu kwa ajili ya kukamilisha mchakato huo na mwekezaji amekamilisha kwa upande wake lakini upande wa mashabiki umekwama.

Akizungumza jana jijini Dodoma, Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Erio alisema anashangazwa na kinachozungumzwa sasa kwenye vyombo vya habari kuwa mwekezaji amekwamisha uwekezaji huo.

Alisema mwekezaji kwa upande wake alitekeleza kile alichotakiwa kufanya kukamilisha mchakato huo na upande wa wanachama nao walipewa mambo ya kuyakamilisha lakini mpaka sasa wameshindwa.

"Nakumbuka wiki mbili zilizopita nilipata barua kutoka RITA (Wakala wa usajili, Ufilisi na Udhamini) walikuwa wamewaita Simba upande wa klabu, siyo upande wa mwekezaji kwa sababu kwenye mkataba kulikuwa na majukumu ya mwekezaji na yale ya klabu kuweka sawa kuelekea katika Simba Sports Club Limited, mwekezaji ana ya kwake na hawa wengine kwa upande wa wanachama wanatakiwa kuweka hati ya jengo la klabu na mali nyingine, vyote hivi vinatakiwa vitoke mikononi mwa klabu na viende mikononi mwa Simba Sports Club Limited, walikuwa wameitwa RITA kwa ajili ya kuendelea kukamilisha hilo zoezi," alisema Mkurugenzi Mkuu huyo.

Alisema katika makubaliano hayo kila upande unatakiwa kukamilisha majukumu ambayo waliagizwa kuyafanya ili mchakato ukamilike.

"Sijafuatilia nini kilitokea baada ya hapo lakini nilipata taarifa kuwa upande wa klabu uliitwa kwenda kuhakikisha, kuambiwa makubaliano yale yana pande mbili kuna upande mmoja chini ya Baraza la Wadhamini halafu upande wa pili ni wa Mwekezaji, wote wana kitu cha kufanya katika hili, bahati mbaya sana kinachozungumzwa sana kwenye vyombo vya habari ni yale majukumu ya mwekezaji na hakuna anayeangalia katika hili Simba nao wanatakiwa wafanye nini lakini katika hicho wanachotakiwa kufanya kama Baraza la wadhamini nalo linaendelea kushughulikiwa, mwekezaji kwa upande wake alishafanya kile anachotakiwa kukifanya na kilibaki upande wa klabu", alisema.

Alisema kwa upande wao kama FCC walishalifunga jambo hilo kwa kuwa wali-

UKURASA. 23

## Mshambuliaji Yanga aomba muda kuonyesha makali yake

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI mpya wa Yanga, Hafiz Konkoni amesema anahitaji muda kidogo kuzoea mazingira ya Tanzania na Ligi hiyo ili kuanza kuonyesha makali yake kwenye timu hiyo na amekataa kufananishwa na Fiston Mayele.

Nyota huyo amewataka mashabiki wa Yanga kuwa na subira naye na kumuamini yeye na wachezaji wengine ili waweze kufanya vizuri na kusaidia timu kufikia malengo yake msimu ujao wa 2023/2024.

Konkoni raia wa Ghana awali alikuwa chaguo la pili katika mchakato wa usajili nyuma ya Mcameroon, Emmanuel Dikongue, ambaye dili lake lilikufa baada ya kushindwana katika maslahi.

Akizungumza na Nipashe jana, Konkoni, alisema hawezi kujitabilia atafunga mabao mangapi, anachoamini ni kuwa atafanya vizuri hivyo anaomba mashabiki wawe na imani naye.

Alisema atachukuwa muda kiodogo kwa kuwa bado anahitaji kuelewana na wenzake pamoja na kuifahamu vizuri ligi ya Tanzania.

"Lazima nijitume hapa, nifanye vizuri kuisaida Yanga kufikia malengo yake lakini na mimi pia kufikia malengo yangu ya kuendelea kuwemo kwenye kikosi cha timu yetu ya Taifa ya Ghana," alisema Konkoni na kuongeza,

"Kiukweli siwezi kutabiri kuwa nitafunga mabao mangapi japo kazi yangu ni kufunga, naamini mashabiki wa Yanga watafurahi wanapaswa kuwa na imani, sijaja hapa kuziba pengo la Mayele na sipendi kufananishwa naye, alikuwepo hapa na alifanya vizuri, nimekuja kuendeleza furaha ya mashabiki wa timu hii" alisema nyota huyo.

Aliongeza kuwa Mayele alifanya vizuri na anauheshimu mchango wake kwenye timu hiyo ila amekuja nchini kuisaidia Yanga kupata matokeo mazuri na kufikia malengo yake msimu ujao na sio kufananishwa na mshambuliaji

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042